KUTATHIMINI VIPENGELE VYA FASIHI SIMULIZI KATIKA UANDISHI WA EBRAHIM HUSSEIN

SALUM ABDALLAH

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii iitwayo: *Kutathmini Ufasihi Simulizi katika Uandishi wa Ebrahim Hussein: Mfano wa Mashetani, Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

_____

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

Tarehe: _____

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

.

TAMKO

Mimi **Salum Abdallah**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

Saini ……

Tarehe ……

TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwanza, kwa baba yangu mpendwa Abdallah S. Kitabuge na Mama yangu mzazi Salama A. Kiseyo, kwa kujinyima na kunipeleka shule. Pili mke wangu Mriam Omari na mdogo wangu Rashidi, kwa mawazo yao mazuri kuhusu taaluma ya Kiswahili. Tatu, mke wangu mpendwa na mwanangu Tausi Salum kwa kunitia moyo hata palipokuwa na matatizo. Mwisho ni mkuu wangu wa kazi katika chuo cha ualim Butimba kwa kunipa ruhusa ya kuhudhuria masomo yangu, Mungu ambariki sana.

SHUKRANI

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu wote ambao kwa namna moja ama nyingine wametoa mchango wao wa hali na mali ambao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha utafiti huu. Nitakuwa mwizi wa fadhira kudai kwamba jitihada zangu pekee ndizo zimeniwezesha kuufanikisha utafiti huu. Ni dhahiri kuwa bila ya ushauri, usaidizi, muongozo na mchango wa watu hawa, tasnifu hii isingekamilika kwa wakati. Si rahisi kuwataja wote bali nitawataja baadhi tu.

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa siha njema na kuniwezesha kutimiza ndoto yangu ya siku nyingi ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Naamini kuwa kutunukiwa shahada hii kutakuwa chachu itakayochachua hali ya kujitaalimisha zaidi katika uga huu wa fasihi ya Kiswahili.

Pili, shukrani zangu za dhati zimuendee msimamizi wangu Mohamed Omary Maguo, kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu kuanzia hatua ya awali kabisa ya kuandaa mada ya utafiti, pendekezo la utafiti, ukusanyaji wa data, uchambuzi na hatimaye kuikamilisha ripoti hii ya utafiti. Katika kipindi chote hiki hakuchoka kuniongoza, kunikosoa na kunishauri katika wakati wote nilipohitaji msaada kutoka kwake. Ama kwa hakika ushauri na mwongozo thabiti wa Dr. Mohamed Omary Maguo ndiyo ulioniwezesha kufanikisha kazi hii. Daima nitaishi nikikukumbuka kwa wema wako. Mwenyezi Mungu akubariki sana na kukujalia maisha marefu yenye kutukuka.

Tatu, shukrani zangu maalumu ziwaendee wahadhiri walionifundisha na kunifungua macho katika ulimwengu wa wasomi kwa njia za kipekee ambao walijitolea na kuhakikisha kuwa nimepata shahada hii ya uzamili. Wanazuoni hao ni Sheikh. Dkt. Prof. T.S.Y.M Sengo, Prof. E. Mbogo, Prof. J.S. Mdee, Dr. A. Kishe, Dr. H. Jilala, Dkt. P.P.P Lipembe, Dkt. H. Simpasa, Dkt. Z. Elisifa na Dr. M.O Maguo. Mungu awabariki kwa fadhira mlizonitendea.

Nne, napenda kuishukuru familia yangu kwa msaada wa hali na mali katika kipindi chote cha masomo yangu. Hasa mke wangu Mariam Omari na watoto wangu wapendwa Tausi Salum,Abdallah Salum na Salama Salum ambao walikosa baadhi ya huduma muhimu wakati wa masomo yangu lakini walinivumilia na kunipa msaada pale nilipokuwa na uhitaji. Nawapenda sana na Mungu awajalie afya njema ili na nyinyi siku moja muweze kufikia hatua hii ambayo mimi baba yenu nimeifikia. Mwisho lakini si kwa umuhimu napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana bega kwa bega kwa kipindi chote cha masomo. Orodha ni kubwa lakini natamatisha kwa kuwashukuru wanafunzi wafuatao: Mwl. Sr. Bwelele, Mwl. Sr. Mgimba, Mwl. Sina, Marehemu Mwl. Kwisubira, Mwl. Mwakila, Mwl. Kibungu, Mwl. Kaniki na, Mwl. Timanywa. Sina lugha nzuri ya kujieleza hasa kuhusu msaada na ushirikiano wenu mlionipatia wakati wa masomo yangu ila nawaombea dua njema kwa Mola wetu.

IKISIRI

Utafiti huu umetathmini ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein: Mfano wa *Jogoo Kijijni, Ngao ya Jadi na Mashetani.* Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi matatu ambayo ni kubainisha vipengele vya Fasihi simulizi katika tamthiliya za *Jogoo Kijijni*, *Ngao ya Jadi na Mashetani*, mwisho ni kubainisha namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyoibua dhamira na kuendeleza dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule. Katika kutekeleza malengo hayo tuliteua sampuli ya utafiti kwa mbinu ya kusudio. Sampuli hiyo ndiyo iliyotumiwa kukusanyia data ya msingi. Data hizi zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini na kuchambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo. Uhakiki wa data katika Utafiti huu uliongozwa na nadhariya mbili ambazo ni nadhariya ya Vikale ambayo imetumika kubainisha ufasihi simulizi katika tamthiliya teule. Na nadhariya ya Fasihi Linganishi imetumika kulinganisha na kulinganua ufasihi simulizi uliojitokeza katika tamthiliya teule. Matokeo ya uatafiti huu yameonyesha kwamba, mosi kuna ufanano mkubwa wa utumizi wa vipengele vya ufasihi simulizi katika tamthiliya teule mbapo katika tamthiliya zote tatu Hussein ametumia ngano, majigambo, ishara, mtindo wa kuchanganya tanzu, tashihisi, ushairi mtambaji, wahusika wa fasihi simulizi na mtambaji katika ujenzi wa tamthiliya ya Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.

Pili, Utafiti huu umebaini kuwa utofauti wa utumizi wa vipengele vya ufasihi simulizi umejitokeza kupitia kipengele cha nyimbo na mianzo na miisho ya kifomula. Vipengele hivi ndivyo livyozitofautisha tamthiliya teule.

YALIYOMO

UTHIBITISHO.....ii

HAKIMILIKI.....iii

TAMKO.....iv

TABARUKU.....v

SHUKRANI.....vi

IKISIRI.....viii

SURA YA KWANZA.....1

1.0 UTANGULIZI.....1

1.1 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mashetani.....1

1.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Jogoo Kijijini*.....2

1.2 Muhtasri wa Tamthiliya ya Ngao ya Jadi.....4

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....5

1.4 Tamko La Tatizo La Utafiti.....7

1.5 Malengo ya Utafiti.....8

1.6.1 Lengo Kuu.....8

1.6.2 Malengo mahususi.....8

1.6 Maswali ya utafiti.....9

1.7 Umuhimu wa Utafiti.....9

1.8 Mawanda ya Utafiti.....10

SURA YA PILI.....11

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA.....11

2.1 Utangulizi.....11

2.2 Ufafanuzi wa Baadhi ya Vipengele vya Fasihi Simulizi Vinavyojitokeza katika Fasihi Andishi 11
2.2.1 Nyimbo 11
2.2.2 Misemo 12
2.2.3 Wahusika wa Kifasihi Simulizi 12
2.2.4 Ucheshi 13
2.2.5 Majigambo 13
2.2.6 Tasifida 13
2.2.7 Taswira 14
2.2.8 Methali 14
2.2.9 Tashihisi 15
2.2.10 Kuingiliana kwa Tanzu 15
2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu vipengele vya Fasihi Simulizi katika Uandishi wa Fasihi 16
2.3.1 Pengo la Utafiti 23
2.4 Mkabala wa Nadhariya ya Utafiti 23
2.4.1 Nadharia ya Vikale 24
2.4.2 Nadhariya ya Fasihi Linganishi 27
2.5 Hitimisho 29
SURA YA TATU 31
3.0 MBINU ZA UTAFITI 31
3.1 Utangulizi 31
3.2 Eneo la Utafiti 31
3.3 Usanifu wa Utafiti 31

3.4 Populesheni, Usampulishaji na Sampuli ya Utafiti 32
3.4.1 Populesheni 32
3.4.2 Sampuli ya Utafiti 33
3.4.3 Usampulishaji 33
3.5 Aina za Data Zilizokusanywa 34
3.5.1 Data za Msingi 34
3.5.2 Data za Upili 34
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data 34
3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini 35
3.6.2 Upitiaji wa Nyaraka 35
3.7 Uchambuzi wa Data 36
3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo 36
3.8 Usahihi wa Data 37
3.9 Maadili ya Utafiti 37
3.10 Hitimisho 37
SURA YA NNE 39
4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI 39
4.1 Utangulizi 39
4.2 Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Tamthiliya Teule 39
4.2.1 Matumizi ya Ngano 39
4.2.2 Mtindo wa Kuchanganya Tanzu 41
4.2.3 Mtindo wa Lugha ya Ishara 50
4.2.4 Matumizi ya Wahusika wa Fasihi Simulizi 55

4.2.5 Matumizi ya Mtambaji 57
4.2.6 Mianzo na miisho ya Kifomula 59
4.2.7 Nyimbo 60
4.3 Namna Vipengele vya Fasihi Simulizi Vilivyotumiwa Kuibua Dhamira Mbalimbali Katika Tamthiliya Teule 62
4.3.1 Dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya ya Mashetani 62
4.3.2 Jogoo Kijijini 68
4.3.3 Ngao ya Jadi 71
4.4 Hitimisho 73
SURA YA TANO 75
5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 75
5.1 Utangulizi 75
5.2 Muhtasari wa Tasnifu 75
5.3 Hitimisho 77
5.3.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Tamthiliya Teule 77
5.3.2 Kutofautiana kwa Vipengele vya Fasihi Simuliz katika Tamthiliya Teule ... 78
5.3.3 Dhamira Zinazojitokeza katika Tamthiliya Teule 78
5.4 Mapendekezo 78
MAREJELEO 79

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Sehem hii ya kwanza imeshughulikia usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti yanayojumuisha lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mwisho kuna hitimisho. Utafiti huu umetafiti tamthiliya tatu za mwandishi Ebrahim Hussein ambapo tumeona kuwa ni vema tutoe muhtasari wa kila tamthiliya ili ifahamike kwa wasomaji wa kazi hii.

1.1 Muhtasari wa Tamthiliya ya Mashetani

Tarehe 12 Januari 1964 Serikali ya Sultan wa Zanzibar ilipinduliwa, na Afro-Shiraz Party, chini ya uongozi wa Abeid Karume, ikakamata hatamu ya serikali. Jambo la kwanza lililofanywa na serikali hiyo ya mapinduzi lilikuwa ni kutaifisha mashamba makubwa na kuifanya ardhi mali ya umma. Baadhi ya wale walipoteza milki yao walijisambaza katika miji ya pwani ya Afrika ya Mashariki kama vile Mombasa, Tanga na Dar es Salam. Miongoni mwao ni familia ya Juma.

Dar es Salaam wakati huo, kama miji mingine mikubwa ya Tanganyika, ilikuwa inapokea Waafrika kutoka majimboni, hasa wale waliokuwa na elimu ya Kiingereza na ya Kizungu, kuja kushika madaraka katika serikali mpya ya Tanganyika. Lakini wengi katika wao, chambacho Mwalimu Nyerere, walikuwa ‘Wazungu Weusi’. Watu hawa baada ya kurithi vile vyeo, nyumba na mwenendo ulioachwa na mkoloni, walianzisha ukabaila. Familia ya Kitaru ilikuwa miongoni mwao.

Familia ya Kitaru na familia ya Juma zilikuwa jirani Dar es Salaam, na baina ya Juma na Kitaru, waliokuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu, palikuwa na urafiki shakiki. Lakini tukiitazama migongano na migogoro ya umma wakati huo, tukitupa macho nyuma na kutazama siku zilizopita, tukisikiliza mawazo ya wazee wao, tutaona kuwa urafiki huo ulikuwa kamba ya mvutano. Upande mmoja (ule wa Kitaru) unavutia katika uchumi na siasa, na upande wa pili (ule wa Juma) unavutia kwenye sumu inayotengenezwa na mbaniko wa hali na inayochujwa na akili iliyojaa kumbukumbu za siku za raha zilizopita.

Migongano na migogoro hii iliyainamisha macho ya Juma na Kitaru, wakawa hawaoni kitu isipokuwa nafsi zao. Urafiki wao ukawa wa chuki, na kila kicheko chao kikawa ni kijichozi. Walilolisema silo walilolilkusudia, na walilolikusudia hawakuwa wakilitamka.Wakavumbua mizaha ili waumizane huku wakicheka. Wakafanya na michezo ili wachezane shere; na ndani ya shere hizo wakauficha ukweli wao.

Katika ugomvi wa Juma na Kitaru muna mahaba. Wanagombana ili kutafuta uhusiano ulio na maana. Hili ndilo wanalolisaka. Lakini tufikapo mwisho wa mchezo hatujui kama wasakaji hawa wameuacha masako wao au la. Tunalolijua ni kuwa Juma kaondoka. Je, atausikia wito wa Kitaru au amehiari kuvunja urafiki na kuondoka? Hili ndilo swali. (Muhtasari huu ni kwa mujibu wa utangulizi ulioandikwa katika tamthiliya ya *Mashetani*, 1972: vii-viii).

1.2 Muhtasari wa Tamthiliya ya *Jogoo Kijijini*

Tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* kimsingi, ina simulio kadhaa mchanganyiko. Kwanza,

inazungumzia mkunazi rahmani uliowaletea watu neema na rehema mpaka kulipotokea mbuubuu ulioutambalia mkunazi huo na kuua kisha ukaingia ukaufu mjini. Pia, tamthiliya hii inaeleza kuhusu jogoo aliyewika na kuashiria watu mapambazuko. Hata hivyo, katika mapambazuko hayo, unyayo wa mtu unalilalamikia sikio kuwa akili ambayo unyayo hauikiri imemfunga hata asione mapambazuko hayo. Mapambazuko hayo hayadumu kwani usiku mzuri unaingia ambapo mtu unamkuta usiku huu njiani. Anapofika karibu na ziwa anaanguka kifudifudi. Mapambazuko ya siku inayofuata yanafika ambapo sikio lilizinduka baada ya kusikia radi ipitayo njia. Baada ya mapambazuko, ulimwengu ukawa unaulizana kwanini jogoo hakuwika siku ile kuyanadi mapambazuko?

Tunaambiwa kuwa tamthiliya hii, zaidi ya kuwa na visa mchanganyiko na vilivyoparaganyika, ina matumizi makubwa ya ishara, picha na taswira. Kwa mfano, tunaelezwa kuwa mtu aliyeanguka kifudifudi ilikuwa ni ishara ya kiza kwa wale watu wa mle ndani. Simulio nyingine iliyomo katika tamthiliya hii ni kijana anayeukamata mti na kujirusha kijijini. Kijana huyu alitaka kupita mlangoni kumbe mlango wenyewe ulikuwa umeliwa na mchwa. Inaelekea katika tamthiliya hii kuwa mlango huu ulikuwa ni mlango wa nasaba na hivyo kuliwa kwake kulivunja nasaba kukawa hakuna tena tabaka la watu watukufu au wanyonge na hivyo utu ukaota. Baada ya kuingia nyumbani kijana anakutana na ajuza. Kukutana kwa ajuza na kijana kunampa wasiwasi jogoo ambaye anarandaranda uga mzima huku akiwa na wasiwasi kuhusu ajuza atamwambia nini kijana. Ajuza anamuadithia kijana usuli wa wao kufika pale kijijini kuwa ni kutokana na madhambi waliyoyafanya. Kijana

anaamua kujitoa kafara kuwa malipizo ya madhambi ya ile njia ili kuikomboa jamii yake (Muhtasari huu pia unapatika katika Mmari, 2016).

1.2 Muhtasri wa Tamthiliya ya Ngao ya Jadi

Ngao ya Jadi inaelezea kuhusu kitongoji kiitwacho Masononi ambacho kilikuwa na mali na binti wazuri. Mara Joka la vichwa sabini liitwalo Sesota, linaingia katika kitongoji cha Masononi. Joka hili lilikuwa na tabia ya kuchukua mali na binti mmoja kila mwaka na hivyo kusababisha hofu kubwa kwa wanakijiji. Wanakijiji wanafanya mkutano kujadili jinsi ya kuliondoa joka hilo na kukomesha vitendo vyake. Katika mkutano huo, ajuza anashauri kuwa joka hilo linaweza kuuawa kama atachaguliwa mtemi atakayepambana nalo. Ushauri wa ajuza unafanyiwa kazi na mtemi anachaguliwa na kuanza kupambana na Sesota. Hata hivyo, mara ya kwanza mtemi anapopambana na Joka na kurusha mkuki wake wa niujiza, yanatokea madhara makubwa ambapo watoto ndiyo wanaoathirika zaidi.

Mara ya pili, Joka linapandwa na mori na kutoa miale ya moto inayokitekeketeza kijiji. Katika mapambano hayo, mtemi anafanikiwa kulikata joka kichwa kimoja, jambo linalolifanya joka hilo kutoweka. Kutoweka kwa Joka kunawafanya watu kufurahi na kushangilia ambapo ngoma mbalimbali zinachezwa. Hata hivyo, Joka linamwachia mtemi sumu mwilini mwake. Ili kujitakasa na sumu hiyo, mtemi analazimika kujiondoa kama njia ya kujitakasa. Kuondoka kwa mtemi kunasababisha kuingia kwa kila aina ya ufisadi kijijini Masononi hata ikaonekana kuwa Sesota amerudi na kichwa cha pili. Watu wakakimbilia kwa mtemi kutafuta msaada lakini wakaishia kuivunja ngao ya jadi. Kutokana na hilo, hakukuwa na la kufanya zaidi ya

kusubiri kudhuriwa na Joka Sesota (Muhtasari huu pia unapatika katika Mmari, 2016).

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kabla ya mwanzoni mwa miaka ya 1970 tamthiliya za Kiswahili zilifanana sana na tamthiliya za Kimagharibi kimuundo ambapo tamthiliya ya Kiswahili ilikuwa na hadithi (simulio), vitendo ambavyo viligawanyika katika sehemu zilizoitwa vitendo, mtiririko wa matukio wenye umbo la piramidi (chanzo cha mgogoro, kukuwa kwa mgogoro, kilele, mshuko na suluhisho), waigizaji (wahusika wa hadithi), dayalojia (mazungumzo ya wahusika) na mwisho ni jukwa la kutendea. Na tofauti kati ya tamthiliya za Kimagharibi za Kiswahili ilijitokeza katika maudhui tu (Mulokozi, 1999) kwa mfano tamthiliya kama *Wakati Ukuta* (Hussein, 1968), *Alikiona* (Hussein, 1968), *Nakupenda lakini…* (Kuria, 1957), *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (Ngugi, 1961), *Atakiwa na Polisi* (Karutu, 1957) miongoni mwa nyingine muundo wake hautofautiani na ule wa tamthiliya za Kimagharibi. Lakini kuanzia miaka ya 1970 watunzi wa tamthiliya za Kiswahili walianza kujitofautisha na watunzi wa tamthiliya wa Kimagharibi kimuundo na hii ilitokana na kupanuka kwa elimu kulikochagizwa na kuanzishwa kwa kozi za sanaa ya maonyesho katika vyuo mbalimbali ikiwemo chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Watunzi wa tamthiliya za Kiswahili na za Kiafrika zikiwemo wakajifunza tamthiliya mbalimbali duniani ambazo zimekiuka miiko ya utunzi wa tamthilya iliyoasisiwa na Aristotle lakini bado zikakubalika kuwa ni tamthiliya kwa mfano tamthiliya za Ibsen, Chekhov na Shakespeare (Mulokozi, 1996; Samweli, 2013).

Katika kipindi hiki cha miaka ya sabini fasihi ya Kiswahili ilishuhudia kuzuka kwa tamthiliya zilizokiuka miiko ya kiutunzi iliasisiwa na Aristotle ambapo watunzi wa tamthiliya wa Kiswahili walianza kutumia vipengele mbalimbali za fasihi simulizi katika kuumba tamthiliya zao kama vile visasili, visakale, majigambo, utambaji wa kingano, tendi simulizi, nyimbo, ushairi, wahusika wa fasihi simulizi, vitendawili, mianzo na miisho ya kifomula, takriri, taharuki na ucheshi (Mulokozi, 1996; Senkoro, 2011; Samweli, 2013).

Miongoni mwa watunzi wa tamthiliya ambao tamthiliya zao zina vionjo vya fasihi simulizi ni Ebrahim Hussein, Penina Mhando, Emmanuel Mbogo na Mulokozi kwa mfano kuna matumizi ya majigambo katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* (Hussein, 1976), Nyimbo katika tamthiya ya *Pambo* (Mhando, 1975), tendi simulizi katika tamthiliya ya *Sundiata* (Mbogo, 2008) na *Mukwava wa Uhehe* (Mulokozi, 1979), Visakale katika tamthiliya ya *Kinjeketile* (Hussein, 1969), mianzo na miisho ya kifomula katika tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (Ahmed, 1990) wahusika wa kifasihi simulizi katika tamthiliya ya *Tambueni Haki Zetu* (Mhando, 1973), *Sadaka ya John Okello* (Mbogo, 2015) na nyinginezo.

Kutumiwa huko kwa vipengele hivi vya fasihi simulizi na watunzi wa tamthiliya katika utunzi wa tamthiliya zao ndiko kulikowavutia wataalamu wa fasihi ya Kiswahili kutafiti na kuhakiki ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili. Miongoni mwa taalamu waliohakiki na kutafiti ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili ni pamoja na Nkwera (1977), King’ei (1987), Mulokozi (1996), Senkoro (2011), Nicholaus (2011), Samwel (2013) na wengineo. Ingawa wataalamu hawa wa

fasihi wamehakiki na kutafiti ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili lakini tafiti na tahakiki zao zimegusia baadhi tu ya vipengele vinavyodhihirisha ufasihi simulizi katika tamthiliya na kuacha vipengele kadha wa kadha ambavyo ni muhimu sana katika kuonyesha namna ufasihi simulizi unavyojitokeza katika tamthiliya. Pia wataalamu hawa hawakulinganisha wala kulinganua ufasihi simulizi unaojitokeza katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi* na *Mashetani.*

Kwa kuzingatia hoja hii utafiti huu umetafiti vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumiwa na Hussein katika ujenzi wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi* na *Mashetani* ambapo tumelinganisha na kulinganua vipengele hivyo na kisha kubainisha namna Hussein alivyotumia vipengele vya fasihi simulizi katika kuibua na kuendeleza dhamira katika tamthiliya hizi teule.

1.4 Tamko La Tatizo La Utafiti

Utafiti na uhakiki wa vipengele vya fasihi simulizi katika matini za fasihi, umefanywa na watafiti pamoja na wahakiki mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa uchunguzi wao umejikita zaidi katika kuainisha tu vipengele hivyo bila kuonyesha namna watunzi wa matini za fasihi wanavyotumia vipengele vya fasihi simulizi katika kuibua na kuendeleza dhamira katika matini zao kwa mfano Nkwera (1977), Mbughuni (1978), Mwandawiro (1984), King'ei (1987), Mulokozi (1996), Mbatia (1999), Wafula (1999), Senkoro (2011), Maina (2013) na Saleh (2015) wamebainisha tu baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi vinavyotumiwa na watunzi wa tamthiliya na riwaya katika utunzi wa matini zao bila ya kuonyesha namna vipengele hivyo vinavyoibua na kuendeleza dhamira ya matini

husika. Pia, tafiti na tahakiki za wataalamu hawa wa fasihi hazikushughulikia ulinganisho wala ulinganuzi wa vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika matini za fasihi.

Kutokushughulikiwa kwa ulinganishi na ulinganuzi pamoja na kuonyesha namna vipengele vya fasihi simulizi jinsi vinavyoweza kutumiwa na watunzi kuinua na kuendeleza dhamira katika matini zao ndiko kulikomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu ambao umejikita katika kutafiti ufasihi simulizi unaojitokeza ktika uandishi wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Utafiti huu umebainisha kufanana na kutofautiana kwa vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya teule na kisha tumebainisha namna Hussein alivyotumia vipengele hivyo katika kuibua na kuendeleza dhamira katika tamthiliya hizi teule.

1.5 Malengo ya Utafiti

Ni ubainishaji wa suala linalokusudiwa kutekelezwa na mtafiti katika utafiti wake. Katika utafiti huu mtafiti amegawa malengo ya utafiti katika sehemu kuu mbili: lengo kuu na malengo mahsusi.

1.6.1 Lengo Kuu

Utafiti huu unalenga kuchunguza ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein: Mfano wa *Jogoo Kijijni*, *Ngao ya Jadi na Mashetani*.

1.6.2 Malengo mahususi

Utafitifiti huu umeongozwa na malengo mahususi mawili ambayo ni:

i. Kubainisha vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya teule

ii. Kufafanua namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyoibua dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule.

1.6 Maswali ya utafiti

Utafiti huu una jumla ya maswali mawili kama ifuatayo:

i. Je ni vipengele vipi vya fasihi simulizi vinavyojibainisha katika tamthiliya za *Ngao ya Jadi*, *Jogoo Kijijini* na *Mashetani*?

ii. Ni vipengele vipi vya fasihi simulizi vinavyoitofautisha tamthiliya *Ngao ya Jadi*, *Jogoo Kijijini* na *Mashetani*?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakapokamilika unategemewa kuleta umuhimu mkubwa katika taaluma ya Fasihi, mosi Kitaaluma utafiti huu utakapokamilika unategemewa kuongeza maarifa kwa watafiti wapya kwa kutumia kazi hii kuchambua kazi nyingine za fasihi kwa kuangalia ni kwa vipi ufasihi simulizi unajitokeza katika utunzi wa tamthiliya za Kiswahili.

Pili, utafiti huutasaidia kuwapa watafiti wajao maeneo mengine zaidi ya kufanyia utafiti kama huu katika kazi nyingine za Ebrahim Hussein ambazo utafiti huu haukuzishughulikia.

Tatu, utafiti huu pia utakuwa chachu itakayo chachua hari ya wataalamu na wanafunzi wanaojifunza tamthiliya ya Kiswahili kufanya tafiti nyingi zaidi juu ya ufasihi simulizi katika uandishi wa tamthiliya za Kiswahili.

Na mwisho lakini si kwa umuhimu utafiti huu utawasaidia waandishi chipukizi wa tamthiliya ya Kiswahili kuvifahamu vipengele vya fasihi simulizi vinavyoweza kutumiwa kuibua na kuendeleza maudhui katika tamthiliya zao.

1.8 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kutathmini ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi na Mashetani* ambapo utafiti huu umebainisha uhusiano na utofauti wa utumizi wa vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya hizi teule. Katika kubainisha uhusiano na utofauti huo, utafiti huu umejikita katika vipoengele vya ushairi, nyimbo, ngao, wahusika wa kifasihi simulizi, methali, nahau, misemo, utambaji wa kifasihi simulizi, mianzo na miisho ya kifomula na takriri. Pia utafiti huu umebainisha namna vipengele hivi vya fasihi simulizi vilivyotumiwa na Ebrahim Hussein katika kuibua dhamira za tamthiliya hizi teule.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii ya pili inawasilisha mapitio ya kazi tangulizi na nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Mapitio ya kazi tangulizi ni usomaji wa kihakiki wa kazi zilizotangulia na zinazofanana au kuhusiana na mada ya utafiti inayokusudiwa kutafitiwa. Hivyo, katika sura hii tumejadili kwa kina machapisho ya kitaaluma yanayohusiana na mada hii ya utafiti. Pia katika sura hii tumejadili kwa kina juu ya nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data.

2.2 Ufafanuzi wa Baadhi ya Vipengele vya Fasihi Simulizi Vinavyojitokeza katika Fasihi Andishi

Sehemu hii imefafanua kwa kina baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi vinavyotumiwa na watunzi wa matini za fasihi katika kuumba matini zao. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni hivi vifuatavyo:

2.2.1 Nyimbo

Mulokozi (1996) anasema, wimbo ni kile kinachoimbwa. Wamitila (2003) anaongezea kwa kusema, nyimbo ni tungo zenye maadhi ya sauti inayopanda na kushuka na huundwa kwa kugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Na hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au wizani. Wamitila (keshatajwa) anaendelea kufafanua kwa kusema, nyimbo huwa na mawazo mazito na hukusudiwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, mgogoro, kukejeli, kuliwaza,

kubembeleza, kutumbuiza, kuongoa na kuburudisha. Kwa kufahamu umuhimu wa nyimbo katika kazi za fasihi, waandishi wa tamthilya kama ilivyokuwa kwa watambaji wa matini za fasihi simulzi nao wameingiza kijitanzu hiki cha fasihi simulizi katika tamthiliya zao wakiwa na malengo sawa na yale ya watambaji. Kijitanzu hiki kimejitokeza sana katika tamthiliya za Mhando kama vile, *Pambo* (1976), *Nguzo Mama* (1982) na *Lina Ubani* (1984).

2.2.2 Misemo

Wamitila (2003) anaeleza kuwa, misemo ni neno lenye upana na huweza kutumiwa kuelezea matamko au kauli fulani zinazoelezea ukweli fulani. Misemo ni mojawapo ya kijitanzu cha fasihi simulizi kinachojitokeza katika tamthiliya ya Kiswahili ambacho hutumiwa kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno, kupamba lugha na mengineyo.

2.2.3 Wahusika wa Kifasihi Simulizi

Msokile (1992, 1993) na Senkoro (2011) anaifasili dhana ya wahusika kama watu, wanyama au vitu katika kazi ya sanaa ya kifasihi waliokusudiwa wawakilishe dhana, mawazo au tabia za watu. Wahusika wanaojitokeza sana katika matini za fasihi simulizi ni wahusika mseto yaani katika hadithi msikilizaji anakutana na wahusika binadamu na wasiokuwa binadamu mathalani majini, mashatani, mazimwi, wanyama, mawe na wengineo. Wahusika wa aina hii wanajitokeza pia katika tamthiliya ya Kiwahili kwa mfano katika *Sadaka ya John Okello* Mbogo ametumiwa wahusika mazimwi ambao kimsingi ni wahusika wa kifasihi simulizi.

2.2.4 Ucheshi

Senkoro (2011) anaeleza kuwa ucheshi ni mbinu ya kifani mbayo wasanii huitumia katika kazi zao za fasihi, kwa lengo la kuzichekesha hadhira zao, au walau kuzifanya hadhira hizo zitabasamu; aghalabu mbinu hii hutumiwa kwa lengo la kuwafurahisha wasomaji, wasikilizaji au watazamaji wa kazi ya fasihi, kuepusha uchovu kwa hadhira au hata kujenga kejeli katika kazi zao. Watunzi wa tamthiliya ya Kiswahili wameiingiza mbinu hii ya ucheshi katika tamthiliya zao wakiwa na malengo sawa na yale ya watunzi wa matini za fasihi simulizi.

2.2.5 Majigambo

Mulokozi (1996) kama alivyonukuliwa na Samweli (2013) anafafanua kuwa majigambo ni mtindo wa kisanii wa kusimulia kwa njia ya kujinaki au “kujikweza” kwa mtu au kitu kuhusu matendo na mambo muhimu ya kishujaa na ya kishupavu aliyoyafanya kwa uwezo wake au kwa nasaba yake. Kijitanzu hiki cha fashi simulizi kimejitokeza sana katika tamthiliya ya Kiswahili ambapo majigambo yametumiwa na watunzi wa tamthiliya kuwajenga wahusika wao kwa mfano kupitia majigambo Mbogo ameweza kumjenga vyema msuhusika John Okello katika tamthiliya ya *Sadaka ya John Okello*.

2.2.6 Tasifida

Hii ni tamathali ya semi inayotumika kupunguza makali ya jambo linalosemwa (Senkoro, 2011). Kwa upande wa Wamitila (2008:396) anaongezea kwa kusema kuwa hii ni mbinu inayotumiwa katika kazi za kifasihi (na maongezi au lugha ya kila siku) kuficha ubaya, uozo au uovu fulani kwa kutumia maneno au lugha ambayo

inapunguza makali ya uozo, ubaya au uovu unaozungumzwa. Si kila neno linapaswa kutamkwa kama lilivyo adabu hii ya lugha katika fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi kwani watambaji wa hadithi huwa na adabu katika lugha yao aghalabu huwa na desturi ya kupunga ukali wa maneno wanayoyatamka katika utambaji wao. Kwa kuwa waandishi wa tamthiliya ni zao la jamii na wao wamejikita wakifuata desturi hii ya kiungwana kwa kutumia tasifida katika uandishi wa tamthiliya zao.

2.2.7 Taswira

Kwa mujibu wa Msokile (1993) na Senkoro (2011) taswira ni mkusanyiko wa picha zinazoundwa na maelezo ya msanii katika kazi yake. Mbinu hii imetumiwa sana na watambaji wa matini za fasihi simulizi katika kuumba picha mbalimbali katika matini zao wanazoziwasilisha kwa hadhira. Watunzi wengi wa matini za fasihi andishi wamekuwa wakitumia mbinu hii katika utunzi wa matini zao kwa lengo kama lile la watambaji wa matini za fasihi simulizi yaani kuwafanya wasoaji wa matini zao kuumba picha mbalimbali katika fikra zao wakatia wanaposoma matini zao.

2.2.8 Methali

Simiyu (2011) anabainisha kuwa methali ni semi fupi zinazosheheni fumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu. Anaendelea kufafanua kwa kusema, methali huwa na lugha teule iliyofumbata sitiara, nidaa, tashbihi, taswaira, maswali ya balagha, takriri, mchezo wa maneno, tamathali za semi, tanakali sauti na mbinu za kinudhuma. Simiyu (keshatajwa) anahitimisha kwa kubainisha umuhimu wa mathali ambao ni kupamba lugha, kuelimisha jamii, kuburudisha, kukosoa, kukejeli na

kuwasifu watu katika jamii. Kutokana na umuhimu huu wa methali waandishi wengi wa tamthiliya wamejikuta wakitumia methali katika kuumba kazi zao wakiwa na malengo yanayofanana na ya watambaji.

2.2.9 Tashihisi

Ni aina ya tamathali ya semi ambayo hutumika kuvipa vitu visivyokuwa na uwezo wa kibinadamu kuyatenda matendo ya kibinadamu. Wakati mwingine tamathali hii huitwa fasili ya binadamu kwani katika tamathali hii, vitu visivyo na sifa walizo nazo watu hupewa sifa hizo (Senkoro, 2011:17). Tashihisi ni mbinu iliyotumiwa sana na watambaji wa hadithi za fasihi simulizi katika kuhuisha wahusika vitu, majini, mazimwi, mashatani na madubwana kutenda matendo ya kibinadamu. Mbinu hii pia inatumiwa na baadhi ya watunzi wa tamthiliya katika kuwajenga wahusika wasio binadamu katika matini zao Hussein akiwemo.

2.2.10 Kuingiliana kwa Tanzu

Mwingiliano wa tanzu katika kazi za kifasihi simulizi si jambo geni kwani watunzi hutumia mbinu hii kwa nia mbalimbali, mfano kwa lengo la kuleta msisitizo au kutoa ufafanuzi juu ya suala linalowasilishwa au hata pengine kuondoa uchovu (Senkoro, 2006). Watunzi wa kazi za fasihi andishi nao wameiga mbinu hii ya utunzi wa kazi za fasihi simulizi katika kuandika matini zao za fasihi andishi ambapo waandishi hutumia tanzu zaidi ya moja wanapoandika kazi zao kwa malengo yale yale ya watambaji wa matini za fasihi simulizi. Kwa mfano utanzu anaoandikwa unaweza kuwa ni tamthiliya lakini ndani yake mtunzi anaingiza mashairi, semi, ucheshi na majigambo. Watunzi walio wengi hupenda kuutumia mtindo huu kwa sababu

husaidia kuzifanya kazi zao kuwa na mvuto zaidi kwa wasomaji. Sehemu hii imeangalia kwa kina baadhi tu ya vipengele vinavyodhihirisha ufasihi simulizi katika kazi ya fasihi kwa lengo la kumfanya msomaji aelewe kwa mifano hai juu ya dhana ya ufasihi simulizi katika kazi za fasihi. Katika, sehemu inayofuata tumewasilisha kazi tangulizi ambazo kwa namna moja au nyingine zimezungumzia ufasihi simulizi katika kazi za fasihi andishi.

2.3 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu vipengele vya Fasihi Simulizi katika uandishi wa Fasihi

Wataalamu mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili wametafiti na kuhakiki ufasihi simulizi unaojitokeza katika uandishi wa matini za fasihi andishi miongozi mwao ni Nkwera (1977), Mbughuni (1978), Mwandawiro (1984), King'ei (1987), Mulokozi (1996), Mbatia (1999), Wafula (1999), Murithi (2002), Senkoro (2011) na Maina (2013). Maandiko ya watafiti na wahakiki hawa yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuonyesha namna watunzi wa matini andishi za fasihi ya Kiswahili wanavyotumia matini na mbinu za fasihi simulizi katika kujenga kazi zao. Sehemu hii imejadili kwa kina makala na tafiti hiz na kwa kuanza mjadala wetu tuangalie makala ya Nkwera:

Nkwera (1977) katika makala yake yenye anuani ya "Ebrahim Hussein mwandishi wa tamthiliya" anasema, tamthiliya za awali za Hussein zilionyesha athari ya Breitch katika utunzi wake lakini kadri alivyozidi kukomaa kiuandishi ndivyo alivyoanza taratibu kuchanganya Jadi ya Ufrika katika uandishi wake mathalan, masimulizi, utambaji, mianzo pamoja na miisho ya kifomula. Nkwera (keshatajwa) anahitimisha kwa kusema, ni dhahiri kuwa Hussein ndiye mwandishi wa mwanzo kuzikiuka

taratibu za uandishi za Ki-aristotle kwa kuingiza ujadi wa kiafrika katika tamthiliya zake. Ukichunguza kwa jicho pevu andiko hili la Nkwera (keshatajwa) utabaini kuwa Nkwera (keshatajwa) anajaribu kuonyesha kuwa Hussein ndiye mwandishi wa kwanza wa tamthiliya ya Kiswahili kukiuka miiko ya kiutunzi ya kimagharibi kwa kutia vionjo vya Kiafrika katika kazi zake. Maelezo haya ya Nkwera (keshatajwa) ndiyo yaliyotupa shauku ya kufanya utafiti huu ili kuchunguza na kubainisha ujadi au kwa maneno mengine ufasihi simulizi unaojitokeza katika uandishi wa Ebrahim Hussein kwa kujikita kwenye tamthiliya zake za *Mashetani, Ngao ya Jadi na Jogoo Kijijini*.

Mbughuni (1978) anaeleza kuwa, nathari za kubuni za Kiswahili nchini Tanzania zilianza wakati wa serikali za kikoloni ambapo kulikuwa na haja ya kutosheleza malengo ya kielemu. Maandishi ya kwanza ya kinathari yalikuwa na sifa za fasihi zimulizi. Na kwa kuwa kazi hizo zilikuwa na malengo ya kieleimu ziliyamulika zaidi masuala ya maadili. Maelezo yanayotolewa na Mbughuni (tumeshamtaja) yametusaidia kufahamu kuwa ufasihi simulizi katika matini za fasihi ya Kiswahili ni zao la waandishi wa awali wa riwaya ya Kiswahili kutumia matini za fasihi simulizi zilizopatikana katika mazingira katika kuandika riwaya zao. Katika utafiti huu tumetumia tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* kubaini namna Hussein alivyotumia vipengele mbalimbali vya fasihui simulizi vinavyopatikana katika mazingira yake katika kuumba tamthiliya teule.

Mwandawiro (1984) anaeleza kuwa, binadamu walianza kuwasiliana kwa vitendo na kwa mazungumzo. Fasihi mazungumzo, yaani fasihi simulizi, ndiyo shina na mizizi

ya fasihi andishi. Maelezo yanayotoleza na Mwandawiro (tumeshamtaja) yanatuthibitishia kuwa ufasihi simulizi katika matini andishi za fasihi ni zao la matini za fasihi simulizi. Katika utafiti huu tumethibitisha dai hili kwa kurejea tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

Mlacha na Madumulla (1986) wanabainisha kuwa, katika kuzungumzia historia ya riwaya ya Kiswahili ni muhimu kuhusisha sanaa na fasihi simulizi. Wanaendelea kufafanua kwa kusema, uhusiano huu sio wa kimuundo, ingawa muundo wa masimulizi ulichangaia kwa kiasi kikubwa katika riwaya nyingi za mwanzo. Maelezo yanayotolewa na wataaalamu hawa yanatuthibitishia kuwa ufasihi simulizi unaojitokeza katika matini za fasihi ni zao la uigaji wa mbinu mbalimbali za utunzi za fasihi simulizi uliofanywa na watunzi wa awali wa riwaya kwa mfano mbinu ya usimulizi katika riwaya ya Kiswahili imeigwa na watunzi wa mwanzo wa riwaya ya Kiswahili kutoka katika fasihi simulizi. Maelezo ya wataalamu hawa yaliamsha ari ya kufanya utafiti huu ili kubainisha namna ufasihi simulizi unavyojitokeza ktika uandishi wa Ebrahim Hussein kwa kujikita kwenye tamthiliya zake za *Mashetani, Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

King'ei (1987) katika makala yake yenye anuani ya "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein" anabainisha kuwa Hussein ndiye mwandishi pekee wa tamthiliya aliyefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia vijitanzu vya fasihi simulizi kama vile ngano na vitendawili katika utunzi wa tamthiliya zake za *Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini*. King'ei (keshatajwa) anahitimisha kwa kusema, *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* ni tamthiliya ambazo zimeathiriwa sana na kumbo za fasihi simulizi.

Andiko hili la King’ei (keshatajwa) limetufaa sana katika utafiti wetu kwani limetusaidia kufahmu kuwa Hussein ametumia vitendawili na ngano katika utunzi wa tamthiliya zake za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Katika utafiti huu sisi tumetafiti na kubaini vijitanzu vilivyotumiwa na Huseein katika utunzi wa tamthiliya hizi na kisha kuonyesha namna Hussein alivyotumia vijitanzu vya fasihi simulizi katika kuibua na kuendeleza maudhui katika tamthiliya zake.

Mulokozi (1996) anasema, kabla ya mwaka 1970 umbo au sura ya tamthiliya ya Kiswahili ilifanana sana na ile ya kimagharibi tofauti ilikuwa ni lugha na maudhui tu. Lakini kuanzia miaka ya 1970 watunzi wa tamthiliya ya Kiswahili walianza kuchota malighafi zao za utunzi kutoka katika sanaa za jadi za Kiafrika. Miongoni mwa waandishi wa mwanzo wa tamthiliya ya Kiswahili waliotumia vionjo vya jadi katika kutunga tamthiliya zao ni Ebrahim Hussein ambaye alitumia mbinu ya utambaji katika utunzi wa tamthiliya zake za *Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini*, Penina Mhando alitumia mbinu ya utambaji katika utunzi wa tamthiliya zake za *Lina Ubani* na *Nguzo Mama*. Mbinu ya majiganbo ilitumiwa na Mhando, Balisidya na Amandika katika utunzi wa tamthiliya ya *Harakati za Ukombozi* na Mbogo katika utunzi wa tamthiliya yake ya *Sundiata*. Kwa upande wa Mulokozi yeye alitumia mbinu ya tendi-simulizi kutunga tamthiliya yake ya *Mukwava wa Uhehe*. Maelezo yanayotolewa na mtaalamu huyu yanatuthibitishia kuwa ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili ni juhudi za waandishi wa tamthiliya wa Kiswahili kutaka kujitofautisha na watunzi wa tamthiliya wa Kimagharibi. Maelezo haya yametufaa sana katika kukamilisha malengo ya utafiti wetu kwani yametusaidi kufahamu kuwa Hussein

ametumia mbinu ya utambaji katika kutunga tamthiliya zake za *Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini.*

Mbatia (1999) anaeleza kuwa dhamira ya maadili ilitawala sehemu kubwa ya fasihi kwa sababu moja wapo ya malengo ya fasihi simulizi ni kuhimiza maadili miongoni mwa watu katika jamii anaendelea kufafanua kwa kusema, kwa vile Shaaban Robert anaweza kuchukuliwa kuwa mwasisi wa fasihi ya kubuni ya kinathari ya Kiswahili, ni mwandishi wa kwanza wa riwaya ya Kiswahili ambaye ameathiriwa na elementi ya kimaadili ya fasihi simulizi. Mbatia (keshatajwa) anahitimisha kwa kusema kuwa, kazi za mwanzo za Shaaban Robert zina uwiano mkubwa na fasihi simulizi. Maelezo yanayotolewa na mtaalamu huyu wa fasihi yanathibitisha kuwa kuna ufasihi simulizi katika matini za fasihi andishi ya Kiswahili. Katika utafiti huu sisi tumethibitisha namna ufasihi simulizi unavyojitokeza katika uandishi wa Ebrahim Hussein kwa kujikita kwenye tamthiliya zake za *Mashetani, Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini*.

Wafula (1999) anabainisha kuwa, Hussein ndiye gwiji la utunzi wa tamthiliya za Kiswahili, ugwiji wake unathibitishwa na utunzi wa tamthiliya ya Mashetani ambayo imeonyesha kwa mafanikio makubwa jinsi mapokeo ya Kiafrika yanavyoweza kutumika pamoja na mbinu za kisasa kufanikisha malengo ya kijukwaa. Wafula (keshatajwa) anaenda mbele zaidi kwa kusema, tamthiliya ya Mashetani ndiyo iliyoweka tarehe mpya katika utungaji wa michezo ya kuigiza katika lugha ya Kiswahili. Maelezo ya Wafula yanatuthibitishia kuwa, Hussein ndiye muasisi wa mabadiliko ya kiutunzi katika tamthiliya ya Kiswahili na hasa ukizingatia kuwa yeye ndiye mwandishi aliyetoa msukumo mkubwa kwa waandishi wa tamthiliya kutumia

vionjo vya fasihi simulizi katika utunzi wa kazi zao. Maelezo ya mtaalamu huyu yametupa hamasa ya kujitoma katika utafiti huu ili kubainisha namna Hussein alivyokuwa bingwa katika kutumia vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi katika ujenzi wa tamthiliya zake za *Mashetani*, *Ngao ya Jadi na Jogoo Kijijini*.

Senkoro (2011) anatumia tamthiliya ya *Lina Ubani* (Mhando, 1984), *Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini* (Hussein, 1976) pamoja na riwaya ya *Rosa Mistika* (Kezilahabi, 1978) kubainisha ufasihi simulizi unaojitokeza katika matini za fasihi ya Kiswahili kwa kutaja baadhi ya vijitanzu vya fasihi simulizi pamoja na miundo ya ngano za fasihi simulizi inayojitokeza katika fasihi andishi ya Kiswahili. Vijitanzu na miundo ya ngano za fasihi simulzi vinavyobainishwa na Senkoro (keshatajwa) katika makala yake ni pamoja na mianzo na miisho ya kifomula, uelezwaji na utambaji, sifa anazopaswa kuwa nazo mtambaji, hadhira na nafasi yake katika uelezaji/ utambaji, marudiorudio, taharuki, ucheshi, tanakali sauti, taswira na ishara, kuingiliana kwa tanzu, muundo na majina ya wahusika. Makala hii ya Senkoro (keshatajwa) imetoa mchango mkubwa sana katika kukamilisha malengo ya utafiti wetu kwani imetusaidia kufahamu kwa kina baadhi ya vipengele na miundo ya fasihi simulizi inayotumiwa na watunzi wa matini za fasihi katika kuumba matini zao.

Maina (2013) anabainisha kuwa, riwaya ya *Utubora Mkulima* imesheheni athari za kimtindo za fasihi simulizi tangu mwanzo hadi mwisho; anaendela kueleza kwa kusema, Riwaya hii inaanza kwa mtindo wa kimasimulizi kwa mfano “Baada ya kutoka Burma, siku moja …” Maina (keshatajwa) anaendelea kufafanua kwa kusema, athari zingine za kimtindo ni ugawaji wa riwaya ya *Utubora Mkulima* katika

mada ndogo ndogo kama vile Kuacha Kazi, Nuru Ndogo, Bihaya na kadhalika na kisha mwandishi kutoa maelezo yanayohusu kila mada. Mtindo huu unadhihirisha athari za fasihi simulizi. Hali kadhalika athari hizi za fasihi simulizi zinaonekana mwishoni mwa riwaya hii ambapo Shaaban Robert anakamilisha riwaya yake kwa kuandika “Hapo ndipo pahali pa kuishia hadithi hii …” Mbinu hii hutumika sana katika kutamatisha hadithi katika fasihi simulizi. Maina (keshatajwa) anahitimisha kwa kusema, matumizi ya tamathali za lugha kama vile methali, tashbihi, taswira, mbinu rejeshi, kinaya, taharuki na nyinginezo ni sababu tosha ya kudai kuwa riwaya ya *Utubora Mkulima* imeathiriwa kwa kiwango kikubwa na fasihi simulizi. Maelezo yanayotolewa na mtaalamu huyu yametusaidia kupanua uelewa wetu kuhusu ufasihi simulizi katika matini za fasihi andishi kwamba unatokana kaida ya watunzi wa matini za fasihi kutumia tanzu, vjitanzu na miundo mbalimbali ya fasihi simulizi katika kuumba matini za fasihi andishi. Katika utafiti huu sisi tumitumia tamthiliya tatu za Hussein kubainisha namna Hussein alivyotumia tanzu, vijitanzu na miundo mbalimbali ya fasihi simulizi katika kuumba tamthiliya zake za *Mashetani*, *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*.

Salim (2015) katika tasnifu yake yenye anuani ya “Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert: Mifano kutoka *Adili na Nduguze* na *Wasifu wa Siti binti Saad*” anaeleza kuwa Shaaban Roert ametumia vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi katika kuibua na kuendelea maudhui katika riwaya zake kwa mfano mandhari ya kifasihi simulizi, wahusika wa kifasihi simulizi, ushairi, utani, masimulizi na semi kuibua dhamira ya ukweli wa maisha, ubinafsi, uadilifu, wivu, chuki, upendo, uadui, choyo, ubinafsi, usaliti, uongzozi bora, uhuru katika maamuzi, uadilifu, ujasiri,

ustahaimilivu, uwajibikaji, uadui, huruma, mafanikio miongoni mwa nyingine. Maelezo ya Saleh (keshatajwa) yametufaa sana katika utafiti wetu kwani yametufungua macho na kuweza kuona namna vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi vinavyotumiwa na waandishi wa matini za fasihi katika kuibua dhamira katika matini zao. Katika utafiti huu na sisi tumebainisha namna Hussein alivyotumia tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kuibua dhamira mbaluimbali katika tamthiliya zake za *Mashetani, Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

2.3.1 Pengo la Utafiti

Ingawa watafiti na wakakiki wa fasihi ya Kiswahili wamefanya kazi kubwa katika kuhakiki na kutafiti kuhusu ufasihi simulizi katika fasihi ya Kiswahili kwa mfano Nkwera (1977), Mbughuni (1978), Mwandawiro (1984), King'ei (1987), Mulokozi (1996), Mbatia (1999), Wafula (1999), Senkoro (2011), Maina (2013) na Salim (2015) lakini maandiko yao hayajahakiki wala kutafiti juu ya ulinganishi na ulinganuzi wa ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein katika tamthiliya zake za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Kutokushughulikiwa kwa suala hili ndiko kulikotusukuma kufanya utafiti huu ili kuliziba pengo hili.

2.4 Mkabala wa Nadhariya ya Utafiti

Sehemu hii inahusu ufafanuzi wa nadhariya iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti zilizokusanywa ili kufanikisha kukamilika kwa malengo ya utafiti huu. Nadharia zilizodadavuliwa katika sehemu hii ni nadharia ya Fasihi Linganishi na Nadharia ya Vikale.

2.4.1 Nadharia ya Vikale

Vikale ni nadharia ya uhakiki wa kazi za fasihi ambayo hutumiwa na wahakiki na watafiti wa kazi za fasihi kama muongozo wa kuhakiki na kuchambua data katika tafiti na tahakiki zao. Kuna mitazamo mikuu miwili inayoeleza kuhusu muasisi wa nadharia ya vikale, mtazamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa muasisi wa nadharia ya vikale ni Gustav Jung. Gustav awali alikuwa mwanafunzi wa Sigmund Freud, mtaalamu aliyeasisi taaluma ya uchanganuzi nafsia. Lakini walitofautiana kimawazo juu ya ufasiri wa matukio aliyopitia mhusika mgonjwa anayechunguzwa. Wakati Freud alisisitiza ung'amuzi bwete wa kimazingira Jung yeye alisisitiza juu ya ung'amuzibwete jumuishi.

Baada ya kutengana na Sigmund Freud, Gustav aliendelea na kazi yake ya kuchunguza ndoto na njozi na kuzifasiri. Kutokana na utafiti alioufanya kwa muda mrefu Gustav aliibua dhana ya vikale. Kwa mujibu wa Gustav vikale ni picha kongwe zinazojitokeza mara kwa mara katika kazi ya fasihi. Vikale vinaweza kuwa taswira, wahusika, miundo ya usimulizi, mitindo, ishara, maudhui na kadhia nyinine zinazopatikana katika fasihi popote pale duniani (Njogu na Wafula, 2007).

Jung anadai kuwa mtu na utamaduni wake ni nakala ya binadamu wengine waliokuwepo kabla yake miaka mingi iliyopita. Mtu huyo huathiriwa na jamii inayomzunguka na hawezi kuzikwepa athari za jamii hiyo inayomzunguka. Gustav anaendelea kufafanua kwa kusema matambiko anayopitia mtu mathalan, sherehe za kumpa mtu jina, sherehe za mazishi, sherehe zinazohusiana na jando na unyago miongoni mwa nyingine huathiri maisha ya mtu binafsi.

Gustav alienda mbele zaidi kwa kuugawa ung'amuzibwete wa binadamu katika sehemu kuu mbili sehemu ya kwanza ni ile ya kikale ambayo huhusu mambo yanayojumuisha wanadamu wote ulimwenguni. Gustav anaendelea kufafanua kwa kusema taswira za asili za kumbukumbu zinazorudiwarudiwa kutokana na tajiriba katika maisha ya tangu mababu zetu wa kale ndizo ambazo hurithiwa na kutiwa kwenye ung'amuzibwete jumuishi ambazo hudhihirika katika visaasili, ndoto, mawazo ya binadamu mathalan, katika vipengele vyote katika maisha ya binadamu wote duniani na pia katika kazi za kifasihi na ya pili ni ile inayohusu mtu binafsi ambayo hujumuisha mambo anayoyakumbuka mtu binafsi.

Mtazamo wa pili ni ule unaodai kuwa muasisi wa nadharia ya vikale ni James G. Frazer na hii inatokana na kujitokeza kwa dhana ya vikale katika andiko la Frazer lenye anuani ya *The Golden Bough*. Andiko hili lilipigwa chapa na Chuo Kikuu Cha Cambridge katika idara ya Anthropolojia Linganishi. Katika andiko hili Frazer alifuatailia kwa ukaribu ruwaza za kimsingi za visasili na matambiko ambapo alidai kuwa ruwaza hizo hujirudiarudia karibu katika kila visasili katika tamaduni mbalimbali (Abraham, 1971).

Mtaalamu mwingine ambaye mawazo yake yametoa mchango mkubwa katika kuiwekea mihimili nadharia hii ya vikale ni Northrop Frye ambapo kupitia andiko lake la *Anatomy of Criticism* anabainisha jinsi vikale vinavyohusu kuzaliwa, upanzi wa mimea na majira kama vile kiangazi, kipupwe yanavyoathiri fasihi.

Kwa ujumla, wafuasi wa nadharia ya vikale wanashikilia kwamba umaarufu wa kazi ya sanaa unatokana na wahusika, maudhui na taswira zinazorudiwarudiwa katika

kazi fulani ya fasihi. Baadhi ya wahusika wanaotumiwa kudhihirisha vikale ni kama: jaribosi au nguli anayeandaa safari ambayo mara nyingi huanzia utotoni hadi anapofika utu uzima ambapo safari hii inaweza kuwa ya kikweli pale nguli anapojizatiti kukisaka kitu au kujisaka mwenyewe. Katika nadharia ya vikale, mkinzani wa nguli huwa ni mhusika wa kikale ambaye hujifunga kibwebwe kuiharibu mipango ya nguli kwa kujaribu kumwangamiza. Aghalabu mhusika huyu huwa mzinzi, mlafi na wakati mwingine huwa tajiri. Mpenzi ni kikale, anaweza kutokea kwa sababu ya kumrubuni nguli asiweze kutekeleza mradi wake. Vilevile katika nadharia hii ya vikale mzee mwenye hekima hutokea ili kumwasa nguli ambapo hutumia miujiza au uramli kumsaidia nguli. Pamoja na kutumia wahusika, mkabala wa nadharia ya vikale huangazia maudhui ya wema na uovu, kikale cha mauti miongoni mwa mengine katika jamii (Njogu na Wafula, 2007).

2.4.1.1 Baadhi ya Mihimili ya Nadharia ya Vikale

i. Mhakiki anapohakiki kazi yeyote ile ya fasihi kwa kutumia nadharia hii ya Vikale, kwanza hana budi kuainisha vikale vyote vinavyopatikana katika matini husika kwa mfano kikale cha wahusika, kikale cha usimuliaji, kikale cha kidhamira, kikale cha mpenzi, kikale cha baba na mama, kikale cha taswira na ishra miongoni mwa nyingine.

ii. Baada ya kuainisha vikale vyote vinavyopatikana katika matini husika mhakiki anapaswa aonyeshe umuhimu wa vikale hivyo katika ujenzi wa matini husika kwa kubainisha namna vikale hivyo vilivyotumiwa na mwandishi katika kuibua na kuendeleza maudhui ya kazi yake.

2.4.1.2 Jinsi Nadharia ya Vikale ilivyotumika

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu, mtafiti aliainisha vikale vyote vilivyojitokeza katika tamthiliya teule na kasha kuvitumia vikale husika katika kuonyesha namna mwandishi wa tamthiliya teule alivyovitimia vikale husika katika kuibua na kuendeleza maughui yake.

2.4.2 Nadhariya ya Fasihi Linganishi

Hii ni nadhariya ya uhakiki wa kazi za fasihi ambayo inajihusisha na ulinganishi na ulinganuzi wa kazi za fasihi. Nadhariya hii imewekewa misingi yake na wataalamu wa fasihi wa Uyunani ya kale ambapo ndiko dhana ya fasihi linganishi ilipoasisiwa. Wayunani walikuwa wakijihusisha na ulinganishaji na ulinganuzi wa kazi mbalimbali za tamthiliya kwa lengo la kuchuja na kupata kazi bora zitakazofaa kuonyeshwa kwa hadhira. Katika kipindi hiki cha awali hakukuwa na misingi jumuishi iliyokuwa ikitumiwa na jamii zote ulimwenguni katika kulinganisha na kulinganua matini za fasihi (Ponera, 2014:43-44).

Mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 wataalamu wa Fasihi Linganishi wa Ufaransa walifanya kazi kubwa ya kuyasambaza mawazo haya ya Fasihi Linganishi katika nchi mbalimbali za bara la Ulaya. Mwanafasihi Linganishi wa Kifaransa aliyetoa mchango mkubwa katika kuyasambaza mawazo haya ya Fasihi Linganishi ni Paul Van Tieghem. Baadaye juhudi za Paul Van Tieghem ziliungwa mkono na wataalamu mbalimbali kutoka katika sehemu mbalimbali za Ulaya. Miongoni mwa wataalamu hao ni Hutchenson Macaulay Posnett, Alezander

Veselovsky, Fyodor Buslaev, Johann Wolfgang Von Goethe, Hugo Meltzl de Lomnitz, Steven Totosy de Zepetnek na wengineo (Ponera, 2014:45-46).

Hivyo basi, ni dhahiri kuwa nadhariya ya Fasihi Linganishi imetokana na mawazo ya wanafasihi linganishi kwani mawazo yao ndiyo yaliyoiwekea misingi nadhariya hii kwa mfano andiko la Posnett *Comperative Literature* (1886) na la Zepetnek la *Comperative Literature: Theory, method and Application* (1998) maandiko haya yametoa mchango mkubwa katika kuiwekea mihimili nadhariya hii ya Fasihi Linganishi.

Waitifaki hawa wa nadhariya hii ya fasihi linganishi wanabainisha kuwa ili zoezi la ulinganishi na ulinganuzi wa kazi ya fasihi uwe na ufanisi mhakiki anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Maarifa au ujuzi juu ya vilinganishwavyo
ii. Kuwapo kwa vitu viwili au zaidi vinavyolinganishwa, na
iii. Kuwapo kwa kigezo au vigezo maalumu vya kulinganisha.

Ukiachilia mbali mahitaji haya ya msingi ambayo mhakiki anapaswa kuyazingatia kabla ya kuanza zoezi la ulinganishi na ulinganuzi, Ponera (2014:51-52) anabainisha hatua kadhaa za kufuatwa wakati wa zoezi zima la ulinganishi na ulinganuzi kwa kumnukuu Maho (1991:1). Hatua hizo ni kubainisha sampuli ya vitu vya kulinganishwa na kulinganuliwa, pili ni kufahamu dhana inayolinganishwa, tatu ni kukusanya data; nne ni kubainisha kanuni na taratibu zitakazofuatwa katika kufanya ulinganisho na ulinganuzi, tano ni kubainisha ulinganisho na ulinganuzi na mwisho ni kufafanua matokeo ya ulinganisho na ulinganuzi huo.

2.4.2.1 Jinsi Nadhariya ya Fasihi Linganishi Ilivyotumika

Katika kufanikisha malengo ya utafiti huu mtafiti amefuata hatua za ulinganishi na ulinganuzi kama zilivyobainishwa na Ponera (2014:51-52). Mosi, mtafiti amebainisha Sampuli ya vitu vya kulinganishwa na kulinganuliwa ambapo kulingana na utafiti wetu sampuli zilizotumiwa na mtafiti katika zoezi zima la kulinganisha na kulinganuwa ni tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Pili, mtafiti amejitaalimisha kwa kina baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika tamthiliya ya Kiswahili ambavyo ndivyo vinavyolinganishwa na kulinganuliwa. Tatu, mtafiti amekusanya data za utafiti huu kutoka katika tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Nne, mtafiti amebainisha taratibu zilizofuatwa katika kufanya ulinganisho na ulinganuzi. Katika Utafiti huu, utaratibu uliofuatwa ni ule wa uibuaji, ulinganishaji na ulinganuzi ambapo tulijiegemeza kwenye misingi ya nadhariya ya vikale. Tano, mtafiti amebainisha ulinganisho na ulinganuzi katika sura ya nne. Na mwisho, mtafiti amefafanua matokeo ya ulinganisho na ulinganuzi huo katika sura ya tano.

2.5 Hitimisho

Sura hii imepitia maandiko mbalimbali ya kazi tangulizi kuhusu ufasihi simulizi unaojitokeza katika matini mbalimbali za fasihi kwa ujumla. Mapitio haya yamebainisha kuwa hakuna utafiti wowote ule uliyofanywa kuhusiana na ulinganishi na ulinganuzi wa ufasihi simulizi katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Sehemu hii pia imejadili kwa kina nadhariya zilizotumika katika uchambuzi wa data ambazo ni nadhariya ya vikale na nadhariya ya Fasihi Linganishi. Vilevile tumebainisha namna nadhariya hizi zilivyotumika katika uchambuzi wa

data. Sura inayofuata imewasilisha njia na mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha kwa kina njia na mbinu za utafiti zilizotumika katika zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa. Pia, sura hii imewasilisha mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika utafiti ikiwemo eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji na aina ya data zilizokusanywa. Pia, tumeelezea vipengele vya mbinu za kukusanya data, kuchambua data, usahihi wa data na maadili ya utafiti.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafti huu wa maktabaani ulifanyika katika jiji la Dar es Salaam na jiji la Mwanza. Ukusanyaji na uchambuzi wa data umefanyika katika maktaba za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, maktaba ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania pamoja na maktaba ya Mkoa wa Mwanza. Tumetumia maktaba hizi katika utafiti huu kwa sababu maktaba hizi zina maandiko mengi ya kitaaluma yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti ambayo yametusaidia kukamilisha malengo ya utafiti huu.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni istilahi inayotumiwa kurejelea ramani inayochorwa na mtafiti kuonyesha mpango mzima wa utafiti kuanzia zoezi la ukusanyaji wa data, uchambuzi mpaka uandishi wa ripoti ya utafiti. Kuna aina mbalimbali za usanifu wa

utafiti lakini katika utafiti huu, sisi tumetumia uchunguzi kifani. Robson (2007) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni mbinu ya mpango wa utafiti ambayo hutumika na mtafiti kuteua eneo au jambo maalumu ambalo yeye amelishughulikia katika utafiti wake. Katika utafiti huu tumeteua kazi mbili za tamthiliya za Ibrahim Hussein ambazo ni *Mashatani, Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kjijini* tamthiliya hizi ndizo tulizozishughulikia. Sababu kubwa iliyomsukuma mtafiti kutumia mbinu hii ni kwamba uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu nyingine (Good, 1996).

3.4 Populesheni, Usampulishaji na Sampuli ya Utafiti

Sehemu hii imejedili kwa kina dhana ya populesheni ya utafiti, namna mtafiti alivyoitumia populesheni kupata sampuli ya utafiti na mwisho sampuli ya utafiti imebainishwa.

3.4.1 Populesheni

Newman (2006) anafasili Populesheni kama mkusanyiko wa watu au vitu ambavyo mtafiti anaweza kuvitumia kuunda sampuli atakayoitumia kukusanyia data za utafiti. Kwa kuzingatia hoja ya Newman (2006) Populesheni ya utafiti huu ilikuwa ni tamthiliya saba za Ibrahim Hussein ambazo ni *Alikiona (1967), Kinjeketile (1969), Wakati Ukuta (1971), Mashetani (1971), Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi (1976) Arusi (1980) na Kwenye Ukingo wa Thimu (1988).* Tamthiliya hizi ndizo zilizotumiwa na mtafiti kuteua sampuli ya utafiti.

3.4.2 Sampuli ya Utafiti

Kothari (2009) anafafanua kuwa, sampuli ni kundi dogo la watoa taarifa linalochaguliwa kutoka katika kundi kuu ambalo kwalo, mtafiti hupata data na kutoa hitimisho. Sampuli ya utafiti ni sehemu ya watafitiwa inayoteuliwa na mtafiti kutoka katika populesheni iliyoandaliwa na mtafiti ili itumike katika ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu mtafiti ameteua tamthiliya tatu za Ibrahim Hussein ambazo ni *Mashetani, Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi.* Sampuli hii imeteuliwa kutoka katika orodha ndefu ya tamthiliya zilizoandikwa na Ibrahim Hussein. Sababu iliyomsukuma mtafiti kutumia mbinu ya Usampulishaji kusudio inatokana na ukweli kwamba mbinu hii humpa mtafiti fursa ya kuteua sampuli anayoona kuwa itamwezesha kupata data anazozihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

3.4.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu au watu ili watumike katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote litakalotafitiwa na hasa ukizingatia kuwa ni vigumu kwa mtafiti kutafiti kundi zima (Cohen na wenzake, 2000; Bryman, 2004). Hivyo basi, usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata kundi lengwa litakalotumiwa katika zoezi la ukusanyaji wa data. Kuna mbinu kadha wa kadha ambazo hutumiwa na watafiti katika uteuzi wa sampuli zao za utafiti. Miongoni wa mbinu za usampulishaji zinazotumiwa na watafiti ni pamoja na mbinu ya usampulishaji kusudio, usampulishaji tabakishi, usampulishaji wa kidhamira na usampulishaji wa kinasibu (Kothari, 2014). Utafiti huu umetumia mbinu ya usampulishaji kusudiao katika uteuzi wa sampuli ya utafiti. Ili kukidhi malengo ya utafiti.

3.5 Aina za Data Zilizokusanywa

Utafiti huu umekusanya data za aina mbili; data za msingi na za upili. Data hizi ndizo zilizotumika katika kuyajibu maswali ya utafiti huu na kusaidia kukamilisha malengo ya utafiti wetu.

3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza, na hujulikana kama data halisi ambazo hazijawahi kukusanywa wala kutumiwa na mtafiti mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huo anaokusudiwa kufanywa (Good, 1966). Data za msingi ndizo ambazo hurejelewa kama mali ghafi ya mtafiti. Data hizi ndizo ambazo hutumiwa kuziba pengo la utafiti liloachwa na watafiti wengine waliotangulia (Kombo na Tromph, 2006). Data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi.*

3.5.2 Data za Upili

Data hizi ni zile ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti wengine ambazo zimetumiwa na watafiti tangulizi kujibu maswali ya tafiti zao. Data za aina hii hupatikana kutoka katika Makala, vitabu, majarida, tovuti, tasnifu na machapisho mbalimbali ambayo yanahusiana na utafiti husika. Hivyo basi, mtafiti amekusanya data za upili kutoka katika matini mbalimbali za kifasihi ambazo zinaendana na mada hii ya utafiti.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Hizi ni mbinu au njia zinazotumiwa na mtafiti katika zoezi la ukusanyaji wa data zilizolengwa kuziba pengo la utafiti lililoainishwa na mtafiti katika utafiti husika.

Kuna mbinu mbalimbali ambazo hutumiwa na watafiti katika ukusanyaji wa data miongoni mwa mbinu hizo ni hojaji, uchambuzi wa kimahudhui, usomaji wa makini, upitiaji wa nyaraka na mbinu ya maktabani. Katika utafiti huu tumetumia mbinu ya usomaji makini kukusanya data za utafiti wetu.

3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Hii ni mbinu ya kukusanya data za msingi katika matini za kifasihi kama vile riwaya, ushairi na tamthiliya na machapisho mengine yanayofanana na hayo kwa lengo la kupata data za kukamilisha malengo ya utafiti uliokusudiwa kufanywa (Kothari, 2008). Mbinu ya usomaji makini imetumika katika kukusanya data za msingi katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijni* na *Ngao ya Jadi*. Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data tumefanya mambo yafuatayo: Kwanza kila tamthiliya imesomwa zaidi ya mara tatu kabla ya kuanza kukusanya data ili kuelewa kwa kina vipengele vya fasihi simulizi vinavyojitokeza katika tamthiliya hizo na namna vinavyoibua na kuendeleza maudhui. Baada ya hapo data zilikusanywa na kuhifadhiwa katika shajara maalumu. Data ambazo zilionekana kukaribiana ziliwekwa pamoja ili kuifanya kazi ya upangaji na uchambuzi wa data kuwa rahisi.

3.6.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti ambaye hukusanya machapisho na kuyasoma kwa uzingativu (Kothari 1990). Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam**,** makavazi ya Taasisi za Taaluma ya Kiswahili Ya Kiswahili (TATAKI) na maktaba

ya chuo cha Ualim Butimba. Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasnifu, majarida, vitabu na makala ambazo zilikuwa na uhusiano na mada ya utafiti.

3.7 Uchambuzi wa Data

Silverman (2005) anafafanua dhana ya uchambuzi wa data kama uchanganuzi kuhusiana na upangaji wa data katika ruwaza mbalimbali ili kuweza kuchunguza, kufafanua na hatimaye kutoa hitimisho kuhusu kipengele kinachochunguzwa. Wataalamu wa utafiti wanakubaliana kuwa kila aina ya data za utafiti huchambuliwa kwa mkabala unaoonekana kuwa unafaa kwa data husika na hakuna mkabala jumuishi yaani mkabala ambao unaoweza kutumiwa kuchambulia kila aina ya data. Kwa kulifahamu hili, data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kama ulivyofafanuliwa hapa chini:

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo

Utafiti huu umetumia mbinu ya kimaelezo katika mchakato wa uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka katika tamthiliya teule. John (2007) anaeleza kwamba uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kuona au kusoma kazi ya fasihi tamthiliya ikiwemo, kisha kuelewa maudhui ambayo yamebeba dhamira, falsafa, migogoro, ujumbe na mtazamo/msimamo wa mtunzi. Katika kufanya hivyo pia mtafiti ataelewa matumizi ya lugha, wahusika, mtindo, muundo na mandhari katika kazi anayoisoma, kuisikia au kuitazama.

Katika kufanikisha uchambuzi wa data katika utafiti huu tumefanya yafuatayo. Kwanza tumesoma kwa kina tamthiliya zilizoteuliwa ili kupata data za utafiti. Baada

ya hapo tumezichambua data na kuzitolea maelezo yanayohusu malengo ya utafiti wetu.

3.8 Usahihi wa Data

Usahihi wa data ni utaratibu anaotumia mtafiti katika upatikanaji wa data sahihi na za kuaminika (Cohen na Wenzake, 2000). Katika kuhakikisha kuwa tunakusanya data sahihi katika utafiti wetu, tumetumia mbinu mbili za kukusanyia data ambazo ni upitiaji wa nyaraka na usomaji makini.

3.9 Maadili ya Utafiti

Enon (1998) anasema, “Mkabala wa maadili ya utafiti ni moja wapo ya masuala muhimu ambayo mtafiti anapaswa kuyazingatia kwa uzito wake wakati akifikiria, akipanga, akitekeleza na hata baada ya kukamilisha utafiti wake.” Maadili yanayotakiwa kufuatwa na kuzingatiwa katika utafiti ni kama vile kupata kibali cha kufanya utafiti, kutunza siri za watafitiwa, kuheshimu mipaka ya utafiti kabla na baada ya kukusanya data (Mbogo na wenzake, 2012). Katika utafiti wetu umezingatia maadili yafuatayo katika kufanikisha kuyafikia malengo ya utafiti huu kwa ufanisi mkubwa mosi mtafiti alikuwa na barua iliyokuwa ikimtambulisha na hivyo kuweza kupata kibali cha kutumia maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na ile ya TATAKI, kutokupotosha ukweli na kufuata kanuni za kimataifa katika kutumia maandiko ya kitaaluma ya waandishi mbalimbali.

3.10 Hitimisho

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika zoezi la ukusanyaji na uchambuziwa data za utafiti huu. Tumewasilisha vipengele vya eneo la utafiti,

usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa na mbinu za kukusanyia data. Vipengele vingine ni mbinu ya kuchambua data, usahihi wa data na maadili ya utafiti. Sura inayofuata inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahin Hussein mfano wa *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sura hii ina sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu kulinganisha vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya teule. Sehemu ya pili imewasilisha kutofautiana kwa vipengele fasihi simulizi katika tamthiliya teule. Na sehemu ya tatu imebainisha namna vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumiwa kuibua na kuendeleza dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule.

4.2 Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Tamthiliya Teule

Sehemu hii imejadili kwa kina kufanana kwa vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya teule. Kwa kuwa vipengele vya vya fasihi simulizi viko vingi, utafiti huu umeshughulikia vipengele vya wahusika wa fasihi simulizi, ishara, matumizi ya ngano simulizi na mtindo wa kuchanganya tanzu.

4.2.1 Matumizi ya Ngano

Ngano ni hadithi za kimapokeo ambazo hutumia wahusika wa aina mbalimbali kama vile wanyama, miti au watu kusimulia tukio au kisa fulani chenye mafunzo (Wamitila, 2012). Wamitila (tumeshamtaja) anaenda mbele zaidi kwa kutaja aina mbalimbali za ngano zinazopatikana katika fasihi simulizi ya Kiafrika ambazo ni

ngano za mazimwi au majitu, ngano za usuli, ngano za kishujaa, ngano za hekaya, ngano za wanyama na ngano za mtanziko. Utafiti huu umebaini kuwa Ebrahimu Hussein ametumia ngano za kimafumbo katika uandishi wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani*.Ngano ni kikale ambacho kinatokana na fasihi simulizi ambacho ni miongoni mwa vikale vinavyopendekezwa na nadharia ya vikale. Hizi ni ngano ambazo zimejengwa kwenye misingi ya mafumbo (Wamitila, 2003). Katika kulithibitisha hilo tumerejelea madondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya hizi teule. Tumeanza uwasilishaji wetu na tamthiliya ya *Mashetani* kama ifuatavyo:

Katika tamthiliya ya *Mashetani* Ebrahim Hussein ametumia kikale ngano ya kimafumbo ya kistiara. Istiara ni hadithi ambayo huwa na maana mbili kuu *maana wazi* na *maana fiche* na maana ya wazi huificha maana ya pili ambayo kueleweka kwake huitaji ufahamu fulani wa muktadha wa hadithi yenyewe. Katika istiara wahusika wanaopatikana na matukio yaliyopo huwa kama mlinganisho wa hali nyinginezo, yaani huwa kama sitiari (Wamitila, 2003). Kwa ithibati zaidi tuangalie mfano ufuatao:

> **Kitaru:** Nilikuwa nafikiria hadithi.
> **Mama:** Hadithi!
> **Kitaru:** Hadithi. Bibi yake Juma siku moja alitutolea hadithi; ndiyo nilikuwa naikumbuka.
> **Mama:** Hadithi! Hadithi gani?
> **Kitaru:** Hadithi ya Chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka uko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali shetani (Mashetani, 1970:28).

Ukichunguza kwa jicho la kihakiki istiara hii utang'amua kuwa imefumbata maana mbili, maana ya wazi na maana fiche. Utafiti huu pia umebaini kuwa tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* zina sifa za ngano za kimafumbo za kistiara. Hii inatokana na ukweli kwamba tamthiliya hizi ni istiara na hasa ukizingatia kuwa tamthiliya hizi zimefumbata maana fiche na maana ya wazi na hata wahusika na mazingira yanaopatikana katika tamthiliya hizi ni mlinganisho tu wa hali ya jamii ya mwandishi.

4.2.2 Mtindo wa Kuchanganya Tanzu

Mtindo wa kuchanganya tanzu katika kazi za kifasihi simulizi si jambo geni kwani watambaji hutumia mbinu hii kwa malengo mbalimbali mfano kwa lengo la kuleta msisitizo au kutoa ufafanuzi juu ya suala linalowasilishwa au hata pengine kuondoa uchovu (Senkoro, 2006). Mbinu hii ya kuingiliana kwa tanzu imetumiwa sana na watunzi wa tamthilia za majaribio akiwemo Mhando katika tamthiliya yake ya *Pambo* (1975), *Nguzo Mama* (1982), *Lina Ubani* (1984) na *Tambueni Haki Zetu* (1973) na Mbogo katika *Sundiata* (2009), *Fumo Liongo* (2011), *Sadaka ya John Okello* (2015) na *Nyerere na Safarai ya Kaanaani* (2016). Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumia mtindo huu wa kuchanganya tanzu za fasihi simulizi katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Vijitanzu vya fasihi simulizi vilivyojitokeza kwenye tamthiliya hizi teule ni majigambo, tashihisi, ushairi. Hivi ni vikale ambavyo mwandishi amevitumia kutoka katika fasihi simulizi. Katika kulithibitisha hilo tutarejelea madondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya hizi teule. Na kwa kuanza mjadala wetu tutajadili kwa kina mtindo huu wa kuchanganya tanzu za fasihi asimulizi katika utanzu wa tamthiliya kwa

kudondoa madondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya ya *Jogoo kijijini, Ngao ya Jadi na Mashetani.* Kwa kuanza mjadala wetu tutajadili kwa kina utanzu wa majigambo uku tukionyesha namna utanzu huu unavyozifananisha tamthiliya hizi teule.

4.2.2.1 Majigambo

Utafiti huu umebaini kuwa majigambo ni mojawapo ya kikale ambacho ni kipengele cha fasihi simulizi kinachozifananisha tamthiliya za Ngao *ya Jadi* na *Mashetani* kwa hoja ya kwamba majigamgo yamejitokeza katika tamthiliya mbili tu kati ya tamthiliya tatu tulizozifanyia utafiti. Katika kulithibitisha hili tuangalia mifano ifuatayo kutoka katika tamthiliya hizi teule. Kwa kuanza mjadala wetu tuangalie dondoo lifuatalo kutoka katika tamthiliya ya *Mashetani*.

Katika tamthiliya ya *Mashetani* vikale majigambo yanajitokeza kupitia mhusika Shetani anapojitapa kwa mhusika Binadamu kwa kuseam:

> Unajua mimi nani?
> Mimi shetani.
> Siyo jini wala kuhani.
> Uwezo wangu hauifadhiki.
> Wema wangu hauhisabiki.
> Ubaya wangu hausemeki
> Ninajenga.
> Ninabomoa.
> Ninatukuza.
> Ninadhalilisha nitakavyo.
> Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
> Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi (Mashetani, 1971:1-2)

Katika mfano huu kujinaki kwa mhusika Shetani kuhusu uwezo aliokuwa nao ndiko kunaibua majigambo.

Kwa upande wa tamthiliya ya *Ngao ya Jadi* majigambo yanajidhihirisha kupitia mtambaji ambaye anasimulia matendo ya kishujaa aliyoyafanya mhusika Mtemi alipokuwa akipambana na Joka Sesota. Kwa ithibati zaidi tuangalie maelezo ya mtambaji ambaye anasema:

> Basi
> Kijana mkuki chini ‘kaukita
> Kaukita
> Lile Joka Sesota ‘kaliita
> Akaliita
> Akaliita
> Tena akaliita
> Lakini Sesota kimya hakuitikia
> Mtemi akaanza kuranda
> Mkuki chini ‘nda ukadinda
> Na ume’we ukampanda
> ‘Kitafuta mahali pa kujichomea
> Basi miujiza si hiyo
> Ile ngao ‘likuwa nayo
> ‘Rusha kidaka kwa mayoyo
> Kama mtu na Ruhani aliyejiwa
> Huku atanda
> Huku aranda
> Huku adanda
> Pale kama mpira akijinyambukia
> Muda si muda
> Kikaja kiwingu
> Kiwingu na mwingi ukungu
> Nd’o hapo mtemi siyahi ‘akaitoa
> Mkuki mkononi ukachomoka
> Ukachomoka
> Kiwinguni nda’ ukajichomeka… (*Ngao ya Jadi*, 1976:39-40)

Madondoo haya yanathibitisha kuwa ufasihi simulizi unazifananisha tamthiliya ya Ngao ya Jadi na tamthiliya ya Mashetani na hasa ukizingatia kuwa kipengele hiki cha majigambo kimejitokeza katika tamthiliya zote mbili

4.2.2.2 Ushairi

Ushairi ni sanaa inayotambulishwa na mpangilio maalum wa sentensi au vifungu; mpangilio ambao una mdundo maalum au ruwaza fulani inayounda wizani, lugha ya mkato, mafumbo na mpangilio usio wa kawaida wa vifungu fulani (Wamitila, 2003). Ushairi ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi zinazotumiwa sana na watunzi wa tamthiliya ya Kiswahili katika kuibua na kuendeleza maudhui mbalimbali katika tamthiliya zao.Ushairi ni kikale ambacho waandishi wamekitumia katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Utanzu huu umejitokeza sana katika tamthiliya ya *Fumo Liongo* (Mbogo, 2009), *Nyerere na Safari ya Kaanaani* (Mbogo, 2016), *Lina Ubani* (Mhando, 1976) na nyinginezo. Ushairi uliotamalaki katika tamthiliya za Kiswahili ni ushairi huru. Huu ni ushairi usiofungamana na kiada za kijadi katika utunzi wake kwa hoja ya kwamba hauzingatii urari wa vina na mizani (Kezilahabi, 1974; Topan, 1974; Mulokozi, 1975; Wamitila, 2010). Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumia mtindo wa kikale cha ushairi huru katika utunzi wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na kwa kiasi fulani kuna matumizi ya ushairi huru katika utunzi wa tamthiliya ya *Mashetani*. Katika kulithibitisha hili tutadondoa mifano kadhaa kutoka katika tamthiliya teule inayothibitisha utumizi wa ushairi huru. Kwa kuanza mjadala huu tutaziangalia tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

Kiumbo tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* hazina tofauti kabisa na mashairi huru ya akina Kezilahabi, Kahigi, Mulokozi na Topan miongoni mwa wengine kwa hoja ya kwamba Hussein katika utunzi wa tamthiliya hizi hakuzingatia arudhi ambayo ndiyo inayochukuliwa na wanamapokeo kuwa uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili (Shaaban Robert, 1968; Mathias, 1970; Abdalla, 1973). Ingawa

Hussein amekiuka arudhi lakini kwa kiasi fulani tamthiliya hizi zina urari wa vina vya mwisho na amegawa tamthiliya hizi katika beti ingawa beti zake hazina mishororo inayolingana pia kuna kina bahari. Kwa uthibitisho zaidi tuangalie mifano ifuatayo kutoka katika tamthiliya hizi:

Mtu
‘Nyayo kisogo**ni**
Jicho ardhi**ni**
Ulimi kinywa**ni**
Ukihisabu hatua za hatim**a**
Baina ya unyay**o**
Karibu na siki**o**
Auishi ya malalamik**o**
‘Nyayo litamk**a**
‘Ewe sikio siki**a**;
Mimi mahabusu wa mya**ka**
Wa k’yatu ulichonivi**ka**
Gizani ninadhohofi**ka**
Nataka ona juwa la siku njem**a**
Mimi mahabusu dhalil**i**
Mfungwa wa yako akil**i**
Akili nisiyo ikir**i**
Wala nisyo ikubali nafsi**a**
Nimechoka thama ‘mecho**ka**
Najua jogoo awi**ka**
Lakini mi nakwaruzi**ka**
Katika giza lisilo ‘nufaiy**a**
Humu k’bandani kiyatu**ni**
Naishi gizani tabu**ni**
Nachunika mikwaruzo**ni**
Ninapopambana nah ii duni**a**
‘Kili yatuma mikono**yo**
Kila hiyo kucha ija**yo**
‘Sabuhi ihudhuria**yo**
Katika kiatu kunifungul**ia** (Jogoo Kijijini, 1976:15-16)

Sesota kaja namna ya pi**li**
Kawa mkali ka’ pilipi**li**
Kwa hamaki hasa ukafi**li**
Kitomgoji kwa nguvu akakijili**a**
Akapiga mikambi ya**ke**
Akapumua moto wa**ke**
Kaonyesha asili ya**ke**
Ya ukatili usio na jinsi**a**

Vibanda moto vikawa**ka**
Mashamba yote ‘kalipu**ka**
Watu watoto pia pa**ka**
Walikuwa majivu rundu kubwa moy**a**
Masiki**ni**
Lahaula masiki**ni**
Masiki**ni**
Lahaula masiki**ni**
Vita vya wakuu
Watoto au paka vinawahusu nini?
Kuwa mizo**ga**
Kupikwa kama mbo**ga**
Au kama ule uyo**ga**
Kabla ya maisha ulimini kuyati**a!** (Ngao ya Jadi, 1976:42-43)

Ukichunguza dondoo hili kutoka katika tamthilya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* utabaini kuwa tamthiliya hizi zina umbo la kikale cha ushairi huru kama tulivyotangulia kubainisha hapo juu kuwa Hussein amezigawa tamthiliya hizi katika beti badala ya maonyesho kama ilivyozoeleka katika tamthiliya ya Kiswahili kama tulivyoonyesha katika dondoo la hapo juu. Beti hizo hapo juu zina vina vya mwisho ambapo katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* baadhi ya vina vya mwisho vilivyojitokeza ni *o*, n*i*, *ka*, *li*, *yo.* Na kwa upande wa tamthiliya *Ngao ya Jadi* baadhi ya vina vinavyojitokeza ni pamoja na *li*, *ke*, *ka*, *ni* na *ya*. Katika tamthiliya zote mbili Hussein kwa kiasi kikubwa ametumia kina bahari cha *a*.

Kwa upande wa tamthiliya ya *Mashetani* Hussein pia ametumia ushairi huru kama ilivyokuwa katika *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* japokuwa ni kwa kiasi kidogo sana kwa ithibati zaidi turejelee dondoo lifuatalo:

Shetani: Unajua mimi na**ni**?
Mimi sheta**ni**.
Siyo jini wala kuha**ni**.
Uwezo wangu hauifadhi**ki**.
Wema wangu hauhisabi**ki**.
Ubaya wangu hauseme**ki** (Mashetani, 1970:1)

Dondoo hili linathibitisha kuwa Hussein ametumia ushairi huru katika utunzi wa tamthiliya ya *Mashetani* kwa hoja ya kwamba dondoo hili lina vina vya mwisho japokuwa halina mizani wala beti lakini kiumbo halina tofauti na umbo la shairi huru. Vina vinavyojitokeza katika dondoo hili ni kina *ni*, na kina *ki*. Ni dhahiri kuwa dondoo hili linatuthibitishia kuwa kwa kiasi fulani tamthiliya ya *Mashetani* ina umbo la ushairi huru na hasa ukizingatia kuwa katika tamthiliya hii matumizi ya sentensi fupifupi yametamalaki na hivyo kuifanya tamthiliya hii kuwa na umbo la kiushairi.

Mifano tuliyoidondoa hapo juu kutoka katika tamthiliya tatu teule inathibitisha kuwa uhusiano katika tamthiliya hizi teule unajitokeza kupitia kipengele cha fasihi simulizi cha ushairi kwa hoja ya Hussein katika tamthilya zake zote tatu yaani *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani* Hussein ametumia ushairi kuibua ufasihi simulizi katika tamthiliya hizi.

4.2.2.3 Matumizi ya Tashihisi

Kama tulivyotangulia kufafanua katika sura ya pili kuwa tashihisi ni aina ya tamathali ya semi ambayo hutumika kuvipa vitu visivyokuwa na uwezo wa kibinadamu kuyatenda matendo ya kibinadamu. Tashihisi ni miongoni mwa vikale ambacho mbinu iliyotumiwa sana na watambaji wa hadithi za fasihi simulizi katika kuhuisha wahusika vitu, majini, mazimwi, mashatani na madubwana kutenda matendo ya kibinadamu. Mbinu hii pia inatumiwa na baadhi ya watunzi wa tamthiliya katika kuwajenga wahusika wasio binadamu katika tamthiliya zao miongoni mwao ni Mbogo katika *Sadaka ya John Okello* (2016), Mhando katika *Tambueni Haki Zetu* (1976) na Ngozi katika *Ushuhuda wa Mifupa* (1990). Utafiti

huu umebaini kuwa Hussein ametumia tashihisi katika ujenzi wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Katika kuthibitisha dai hili tuangalie tamthiliya ya *Mashetani*.

Katika tamthiliya ya *Mashetani* matumizi ya kikale tashihisi yanajitokeza kupitia mhusika Juma anapomwambia Kitaru kwa kusema:

> Sasa unaniambia nini. Hujaniambaia kitu. Kweli inauma bwana. Kweli … acha yote hayo. Ukweli bwana, *degree inakupa tonge la wali na mchuzi, tena mchuzi wa kuku, badala ya tonge la ugali na maharagwe* (*Mashetani*, 1971:17).

Katika dondoo hili *degree* imepewa uweza wa kibinadamu yaani kumpa mtu wali na mchuzi wa kuku jambo ambalo kiuhalisia haliwezekana.

Kwa upande wa tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na ile ya *Ngao ya Jadi*, Hussein pia ametumia tashihisi kama kikale katika kuibua na kuendeleza maudhui katika tamthiliya hizi. Ifuatayo ni mifano ya tashihisi inayojitokeza katika tamthiliya hizi kwa kuanza tuangalie tamthiliya ya *Jogoo kijijini*.

> Baina ya *unyayo*
> Karibu na *sikio*
> Auishi ya malalamiko
> '*Nyayo* litamka
> 'Ewe *sikio* sikia;
> Mimi mahabusu wa myaka
> Wa *k'yatu* ulichonivika
> Gizani ninadhohofika
> Nataka ona juwa la siku njema
> Mimi mahabusu dhalili
> Mfungwa wa yako akili
> Akili nisiyo ikiri
> Wala nisyo ikubali nafsia
> Nimechoka thama 'mechoka
> Najua jogoo awika
> Lakini mi nakwaruzika

Katika giza lisilo ‘nufaiya
Humu k’bandani *kiyatuni*
Naishi gizani tabuni
Nachunika mikwaruzoni
Ninapopambana nah ii dunia
‘Kili yatuma mikonoyo
Kila hiyo kucha ijayo
‘Sabuhi ihudhuriayo
Katika kiatu kunifungulia
‘*Nyayo*
Kisogo kikatazama
Kwa fikira kili’nama
Kupima maneno na kuyatazama
Yapoteayo katika hiyo njia (*Jogoo Kijijini*, 1976:15-16)

Katika dondoo hili Hussein ameihuisha *nyao* na kuipa uwezo wa kuyatenda matendo ya kibinadamu kama vile kulalamika kuwa anaonewa na kutaka kupewa uhuru wake. Pia *kisogo* kimehuishwa na kupewa uwezo wa kufikiri kana kwamba ni mwanadamu. Hussein pia ametumia tashihisi katika tamthiliya ya *Ngao ya Jadi* ambapo amelihuisha *Joka Sesota* nakulipa huwezo wa kutenda matendo ya kibinadamu kama vile ufisadi na mengineyo kwa ithibati zaidi tuanagalie dondoo lifuatalo:

Kwani
‘Likuwa tabia makini
Killa mwaka ukibaini
Joka hushuka kijijini
Kuchukua mali na binti Mwema mmoya
Sesota kaja namna ya pili
Kawa mkali ka’ pilipili
Kwa hamaki hasa ukafili
Kitomgoji kwa nguvu akakijilia
Tena ilikuwa fisadi
Mali ya watu tangu jadi
Nao watoto wa Wadudi
Na mshenzi maluuni kuchukuliwa!
Akapiga mikambi yake
Akapumua moto wake
Kaonyesha asili yake
Ya ukatili usio na jinsia (*Ngao ya Jadi*, 1976:35-42)

Madondoo tuliyoyadondoa hapo juu yanathibitisha kuwa kuna ufanano kati ya tamthiliya ya *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani* na hasa ukizingatia kuwa katika tamthiliya zote tatu Hussein ametumia tashisishi kama kionjo cha kifasihi simulizi katika uandishi wa tamthiliya hizi.

4.2.3 Mtindo wa Lugha ya Ishara

Ishara ni alama yenye kuwakilisha au kuashiria kitu fulani (Kamusi ya Kiswahili Sanifu, 2014). Ishara kama kipengele cha fasihi simulizi kimetumiwa kwa umahiri mkubwa na Hussein katika kuibua ufasihi simulizi katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani*. Katika kuishadadia hoja hii tumedondoa dondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya hizi teule. Kwa kuanza mjadala wetu tutadondoa dondoo kutoka katika tamthiliya ya Mashetani linalothibitisha namna ishara ilivyotumiwa na Hussein kuibua ufasihi simulizi katika tamthiliya hii. Kwa ufafanuzi zaidi turejelee dondoo yafuatayo:

> **Kitaru:** Nilikuwa nafikiria hadithi.
> **Mama:** Hadithi! Hadithi gani?
> **Kitaru:** Hadithi ya Chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. *Chewa* huyu akivuta *pumzi maji* yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka uko aliko, kuivuta na kuimeza *mashua* yoyote anayoitaka. *Mashua* inavutwa tu na *mkondo wa maji*, ikitaka isitake. Na huyu *chewa* siyo *chewa* bali *shetani* (*Mashetani*, 1970:28)

Katika dondoo hili neno *chewa* limetumiwa kuashiria mataifa makubwa ya kibepari na *mashua* limetumika kuashiria nchi za dunia ya tatu na neno *pumzi* limetumika kuashiria nguvu za kiuchumi ilizonazo nchi za kimagharibi. Na neno *maji* imetumiwa kuashiria mali ghafi za nchi za dunia ya tatu na kwa upande wa neno

mkondo Hussein amelitumia neno hili kuashiria mfumo wa kibepari unaoziendesha nchi za dunia ya tatu kadri mfumo utakavyo. Tuangalie mfano mwingine uliofumbata ishara kutoka katika tamthiliya hii ya Mashetani.

> **Shetani:** Unajua mimi nani?
> Mimi shetani.
> Siyo jinni wala kuhani.
> Uwezo wangu hauifadhiki.
> Wema wangu hauhisabiki.
> Ubaya wangu hausemeki
> Ninajenga.
> Ninabomoa.
> Ninatukuza.
> Ninadhalilisha nitakavyo.
> Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
> Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi
> Unaniogopa
> **Binadamu:** Ndiyo
> **Shetani:** Unaninyenyekea?
> **Binadamu:** Ndiyo
> **Shetani:** (*kwa ukali*.) Njoo hapa! (*binadamu anakuja*)
> Sivyo, sivyo, sivyo! Sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio*.) Ah, sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa*.) Hebu jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa. Anasujudu*.) Ndiyo, sasa sawa. Hivi sawa sawa. *(Mashetani,* 1970:1-3)

Katika mfano huu wa pili neno *Shetani* ni kikale ambacho kimetumiwa kuashiria uovu au ukoloni mkongwe uliokuwa ukizikandamiza nchi za dunia ya tatu na *Binadamu* ni kikale kinachowakilisha Waafrika waliokuwa wakikandamizwa na kuonewa na ukoloni mkongwe yaani *Shetani*.

Mfano ufuatao nao unadhihirisha namna ishara ilivyotumiwa na mwandishi katika kujenga kazi yake.

> **Shetani:** Rafiki yangu mpenzi, rafiki mwandani. Rafiki wa milele, rafiki wa daima. Ninakupokea. Ninaifurahikia leo, siku ya uzao wako. Kutoka katika *tumbo la giza jeusi*, kuingia katika *ulimwengu wa nuru nyeupe (Mashetani*, 1971:4).

Katika dondoo hili mwandishi ametumia kikale *tumbo la giza jeusi* kuashiria ujinga uliomgubika Mwafrika kutokana na kukosa elimu na kwa upande wa *ulimwengu wa nuru nyeupe* kikale hiki kimetumiwa na mwandishi kuashiria elimu aliyoipata Mwafrika kutoka kwa mkoloni ambayo ndiyo aliyoitumia katika kujikomboa.

Kwa upande wa tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Hussein pia ametumia kipengele cha ishara kama ilivyokuwa katika tamthiliya ya *Mashetani* kuibua ufasihi simulizi katika tamthiliya yake. Kwa kulithibitisha dai hili tutaanza na tamthiliya ya *Jogoo Kijijini*. Kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> Mtu
> ‘*Nyayo* kisogoni
> Jicho ardhini
> Ulimi kinywani
> Ukihisabu hatua za hatima
> Baina ya unyayo
> Karibu na sikio
> Auishi ya malalamiko
> ‘Nyayo litamka
> ‘Ewe sikio sikia;
> Mimi mahabusu wa myaka
> Wa *k’yatu* ulichonivika
> *Gizani* ninadhohofika
> Nataka ona *juwa* la siku njema
> Nimechoka thama ‘mechoka
> Najua *jogoo awika*
> Lakini mi *nakwaruzika*
> Katika *giza* lisilo ‘nufaiya
> Humu k’bandani *kiyatuni*
> Naishi *gizani* tabuni
> Nachunika mikwaruzoni
> Ninapopambana na hii dunia (*Jogoo Kijijini*, 1976:15-16).

Katika dondoo hili Hussein ametumia neno *nyayo* kuashiria Waafrika waliokuwa wakiteseka na utawala wa kidharimu wa kikoloni, neno *sikio* limetumika kuashiria mkoloni ambaye alikuwa akijifanya kuwa hafahamu kuwa dunia imebadilika na kung'ang'ania kuendelea kumtawala Mwafrika. Neno *kiatu* limetumika kuashiria utawala wa kidharimu wa kikoloni ulioanzishwa na mataifa ya kibepari mara tu baada ya mkutano mkuu wa kibepari uliofanyika uko Berlin Ujerumani. Kwa upande wa neno *jogoo awika* limetumiwa na mwandishi kuashiria mabadiliko yaliyoikumba nchi nyingi duniani zilizokuwa chini ya utawala wa kidhalimu wa kikoloni mwanzoni mwa miaka ya hamsini yaliyopelekea kuibuka kwa vuguvugu la harakati za kudai uhuru wa nchi nyingi za Kiafrika. Neno *gizani* ni kikale kilichotumiwa na Hussein kuashiria ujinga ulikuwa umewagubika Waafrika hasa nyakati za utawala wa kidharimu wa kikioloni kwani hata elimu ndogo waliyokuwa wakipewa dabo haikuweza kuwakomboa badala yake ilitumiwa na wakoloni kuendelea kuwakandamiza Waafrika na kuishi katika dhiki kuu.

Kwa upande wa tamthilya ya *Ngao ya Jadi*, Hussein pia ametumia ishara katika kuijenga kazi yake kwa ithibati zaidi tungalie dondoo lifuatalo:

> Hatua si hatua
> Ni mdomo na pua
> Liliishi kitongojini
> Sesota
> Joka la vichwa sabiini
> Rai ikatoka
> Kuwa lile joka
> Damu yake lazima kuimwaya
> Maana ilikuwa dhiki
> Kitongoji hakikaliki
> Maisha yalikuwa siki
> Machungu na makali kwa kila mmoya
> Tena lilikuwa fisadi

Mali ya watu tangu jadi
Nao watoto wa Wadudi
Na mshenzi maluuni kuchukuliwa!

Katika dondoo hili mwandishi ametumia kikale *Sesota* kuashiria ukoloni mkongwe na *siki* ni kikale kilichotumiwa na mwandishi kuashiria ugumu wa maisha ya Waafrika wakati wa utawala wa kidharimu wa kikoloni kwani kila kilichochumwa na Mwafrika hakikumnufaisha hata kidogo bali kilimnufaisha mkoloni. Hata Waafrika walipokata shauri la kuliondoa *Joka Sesota* yaaani mkoloni *Sesota* halikuwa tayari kuondoka likapiga mikambi na kutoa mioto mikali kama asemavyo mtambaji:

Sesota
Kawa mkali ka' pilipili
Kwa hamaki hasa ukafili
Akapiga mikambi yake
Akapumua *moto* wake
Kaonyesha asili yake
Ya ukatili usio na jinsia
Vibanda moto vikawaka
Mashamba yote 'kalipuka
Watu *watoto* pia paka
Walikuwa majivu rundu kubwa moya
Masikini
Lahaula masikini
Vita vya wakuu
Watoto au paka vinawahusu nini? (*Ngao ya Jadi*, 1976:42-43)

Katika dondoo hili neno *moto* umetumika kuashiria nguvu walizokuwa nazo wakoloni ambazo walizitumia kudhibiti harakati za kudai uhuru zilizokuwa zikifanywa na Waafrika. Na neno *wakuu* limetumika kuashiria wakoloni na viongozi walisimama msitari wa mbele katika kuakikisha kuwa bara la Afrika linakuwa huru na neno *watoto* limetumika kuashiria Waafrika waliokuwa wakitawaliwa na Wakoloni ambao ndio waliokuwa wakipata madhara makubwa pindi viongozi wao

walipokuwa wakipambana na wakoloni mfano mzuri ni vita vya Mau Mau vilivyopiganwa nchini Kenya wakati wa utawala wa kikatili wa kikoloni wa Kiingereza walioathirika ni Wakenya ambao waliishi katika kipindi kigumu sana.

Hivyo basi, kutumiwa kwa ishara hizi na Hussein katika tamthiliya hizi teule kunaonyesha namna Hussein alivyokuiwa mahiri katika kutumia vipengele vya fasihi simulizi katika ujenzi wa kazi yake na hasa ukizingatia kuwa chimbuko la matumizi ya ishara katika matini za fasihi andishi ni matini za fasihi simulizi.

4.2.4 Matumizi ya Wahusika wa Fasihi Simulizi

Kama tulivyotangulia kufafanua katika sura ya pili kuwa wahusika ni watu, wanyama au vitu katika kazi ya kifasihi wanaokusudiwa kuwakilisha dhana, mawazo au tabia za watu. Kama tulivyotangulia kusema katika sura ya pili kwamba, katika matini za fasihi simulizi wahusika mseto ndiyo wanaojitokeza sana yaani katika hadithi msikilizaji anakutana na wahusika binadamu na wale wasiokuwa binadamu mathalani majini, mashetani, mazimwi, wanyama, mawe na wengineo. Na wahusika hawa ni vikale ambao wajitokeza karibu katika ngano simulizi za jamii mbalimbali duniani. Utafiti huu umebaini kuwa Wahusika wa aina hii wamejitokeza katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini*, *Ngao ya Jadi* na *Mashetani* ambapo katika tamthiliya zote hizi tatu Hussein ametumia wahusika wa fasihi simulizi. Katika kushadidia hoja hii tutadondoa dondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya zote tatu na kwa kuanza mjadala wetu tutaishughulikia tamthiliya ya *Mashetani*.

Katika tamthiliya ya *Mashetani* Hussein ametumia wahusika wa fasihi simulizi katika igizo linalopatikana katika tamthiliya hii ya *Mashetani* lililoigizwa na mhusika

Juma na mhusika Kitaru ambapo Juma anaigiza kama Shetani na Kitaru anaigiza kama Binadamu. Igizo hili linaigiziwa mbuyuni. Pia katika tamthiliya hii ya *Mashetani* kuna hadithi ya Chewa, hadithi hii alisimuliwa Kitaru na bibi yake Juma. Katika hadithi hii kuna Mhusika Chewa ambaye kimsingi ni mhusika kifasihi simulzi. Pia katika Mashetani kuna mhusika bibi, baba na mama wahusika hawa hujitokeza sana katika hadithi simulizi za kijadi. Wahusika hawa ni vikale kwani aghalabu katika ngano simulizi hadhira hukutana na mhusika bibi, baba, mama, ndege, samaki, wanyama na wengineo. Ni dhahiri kuwa Wahusika hawa wametumiwa na Hussein kwa lengo la kuibua na kuendeleza maudhui katika tamthiliya yake.

Na kwa upande wa tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* Hussein pia ametumia wahusika wa kifasihi simulizi kwa mfano katika tamthiliya ya *Ngao ya Jadi* kuna mhusika Sesota, Sesota ni joka kubwa lenye vichwa Sabini. Sesota ni mhusika wa kingano ambaye amejitokeza kwenye ngano nyingi za Kiafrika tofauti ya Sesota wa Hussein na Sesota wa ngano za kijadi ni kwamba Sesota anayejitokeza kwenye ngano za kijadi huwa na vichwa saba lakini Sesota wa Hussein anavichwa sabini lakini kiwasifu Sesota huyu analandana na sesota wa anayejitokeza kwenye *ngano za kijadi*.

Pia, katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* mtunzi anatumia wahusika wa kifasihi simulzi kama ilivyokuwa katika tamthiliya ya *Ngao ya Jadi* na *Mashetani* kwa mfano katika tamthiliya hii kuna mhusika Jogoo na mhusika bibi kizee (kizee). Wahusika hawa hujitokeza sana katika ngano simulizi za Kiafrika na pia wahusika

hawa ni vikale mathalani mhusika bibi katika fasihi simulizi ambaye ni mhusika kikale huwa na busara sifa hii pia inajitokeza kwa mhusika kizee katika *Jogoo kijijini* mhusika huyu anabusara kama alivyo mhusika bibi katika ngano simulizi. Hivyo basi ni dhahiri kuwa wahusika hawa yaani mhusika Jogoo na Mhusika kizee ni wahusika wa kifasihi simulizi kwani si jambo la kushangaza kwa hadhira kukutana na mhusika ndege au bibi kizee katika ngano za kijadi.

4.2.5 Matumizi ya Mtambaji

Hii ni dhana inayotumiwa kuelezea msimulizi wa hadithi katika fasihi simulizi; yaani anayetamba hadithi. Katika jamii zetu nyingi, watambaji aghalabu huwa watu wazima ingawa zipo hadhira ambako vijana huweza kutambiana ngano wao kwa wao (Wamitila, 2003). Kama tulivyotangulia kuona hapo juu kuwa mtambaji ndiyo msimulizi wa ngano za kijadi za Kiafrika hivyo basi mtambaji ni kikale kwa hoja ya kwamba mtambaji amekuwa akijitokeza kama muwasilishaji wa ngano simulizi katika jamii mbalimbali duniani. Utafiti huu umebaini kuwa Hussein amaetumia mtambaji katika tamthiliya zote tatu katika kulithibituisha hili tutadondoa dondoo kadhaa kutoka katika tamthiliya teule zinazodhihirisha namna Hussein alivyomtumia mtambaji katika kuwasilisha tamthiliya zake kwa kuanza tuangalie tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

Katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*, mtunzi ametumia mtambaji katika kusimulia visa vinavyopatikana katika tamthiliya hizi. Mtambaji anayejitokeza katika tamthiliya hizi anasifa zinazofanana na mtambaji anayejitokeza kwenye ngano simulizi. Kwanza Mtambaji huyu anafanya kazi kubwa ya kusimulia kisa kizima

katika tamthiliya nzima yaani kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa tamthiliya katika tamthiliya zote mbili. Pia mtambaji katika tamthiliya zote mbili anaishirikisha hadhira yake katika uwasilishaji wa hadithi yake kwa kuiuliza maswali hapa na pale mathalani mtambaji anaiuliza hadhira maswali kama aendelee kusimulia kisa au akikatishe na kukimalizia siku nyingine na hadhira inajibu kuwa aendelea. Kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo kutoka katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*.

Katika tamthiliya ya *Mashetani*, Hussein pia anatumia mtambaji ambaye ni mhusika Bibi. Mhusika huyu anawatambia Juma na Kitaru hadithi ya Chewa kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> **Bibi:** Zamani akija hapa, akisikiliza hadithi yeye (Kitaru) na mwenziwe (Juma). Nikiwatambia hadithi hapa wote. (Mashetani, 1970:37)

Hoja hii inashadidiwa na Kitaru kwa ushahidi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> **Kitaru:** Nilikuwa nafikiria hadithi.
> **Mama:** Hadithi!
> **Kitaru:** Hadithi. Bibi yake Juma siku moja alitutolea hadithi; ndiyo nilikuwa naikumbuka.
> **Mama:** Hadithi! Hadithi gani?
> **Kitaru:** Hadithi ya Chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. Chewa huyu akivuta pumzi maji yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka uko aliko, kuivuta na kuimeza mashua yoyote anayoitaka. Mashua inavutwa tu na mkondo wa maji, ikitaka isitake. Na huyu chewa siyo chewa bali shetani (Mashetani, 1970:28)

Kutumiwa kwa mtambaji kusimulia visa vinavyozijenga tamthiliya hizi tatu ndiko kunakothibitisha ufasihi simulizi katika uandishi wa Hussein na hasa ukizingatia kuwa mtambaji ndiye msimuliaji mkuu wa ngano simulizi katika fasihi simulizi

katika jamii mbalimbali dunia. Hivyo basi kikale hiki ndicho kinachozikutanisha tamthiliya hizi tatu na kuzifanya tamthiliya hizi kuwa na kionjo cha Kiafrika.

Hivyo basi, kutumiwa kwa mhusika Joka Sesota katika tamthiliya ya *Ngao ya jadi*, Chewa katika *Mashetani* na Jogoo katika *Jogoo Kijijini* ndiko kunakothibitisha ufasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein katika tamthiliya hizi teule.

4.2.6 Mianzo na miisho ya Kifomula

Watambaji wa ngano simulizi dunia kote huwa na namna fulani ya kuanza na kuhitimisha simulizi zao. Mingoni mwa mianzo hiyo ni Mtambaji kuanza kwa kusema, ‘paukwa’ na hadhira inaitikia kwa kusema, ‘pakawa’, mtambaji anarudia tena kwa kusema, ‘paukwa’ na hadhira hujibu kwa kusema ‘pakawa’ ndiposa mtambaji huanza masimulizi yake kwa kusema, ‘Hapo zamani za kale paliondokea…’ Mwisho mtambaji huitimisha masimulizi yake kifomula mathalani kwa kusema, ‘na hadithi yangu imeishia hapo’ (Wamitila, 2003). Mianzo na miisho hii ya kifomula ni kikale na hasa ukizingatia kuwa karibu katika jamii mbalimbali Afrika watambaji huanza na kumaliza masimulizi yao kwa namna inayofanana. Katika kuleta upya katika uandishi wake Hussein ametia kionjo hiki katika uandishi wa tamthiliya ya Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi kwa hoja Aambapo katika tamthiliya zote mbili mtambaji ameanza na kwa kusema;

Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Hapo kale, palikuwa na Mkunazi

Kiitikio: *Naam twaiib*
Mtambai Hadithi: Mkunazi mkubwa pita kiasi…
(Jogoo Kijijini, 1976:13)

Na kwa upande wa tamthiliya ya *Ngao ya Jadi* mwanzo huu wa kifomula pia unajitokeza kwa ithibati zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Paukwa
Kiitikio: *Pakawa*
Mtambaji Hadithi: Hapo kale
Kiitikio: *Naam twaiib*
Mtambai Hadithi: Hapo kale palikuwa na kitongoji
Kitongoji cha zamani
Te-ena cha zamani… (Ngao ya Jadi, 1976:33)

Watambaji katika tamthiliya zote mbili wanahitimisha visa vyao kifomula kwa kusema:

Basi hapa kadi tamati
Kadi tamati kalimati
Maneno yamenisaliti
Na kisa pia kimenikaukia

Kionjo hiki cha kifasihi simulizi ndicho kinacho zitofautisha tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* na tamthiliya ya *Mashetani* kwa hoja ya kwamba katika tamthiliya ya *Mashetani* kionjo hiki cha kifasihi simulizi hakijatumiwa. Hivyo basi kionjo hiki kinaweka msingi wa kinazitofautisha tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi* na tamthiliya ya *Mashetani.*

4.2.7 Nyimbo

Nyimbo ni mojawapo ya kijitanzu cha fasihi simulizi kinachojitokeza sana katika tamthiliya ya Kiswahili kwa mfano kijitanzu hiki kimejitokeza katika *Pambo*

(Mhando, 1976), *Nguzo Mama* (Mhando, 1980), *Sadaka ya John Okello* (Mbogo, 2015) miongoni mwa nyingine. Utafiti huu umebaini kuwa kijitanzu cha nyimbo kimejitokeza katika tamthiliya ya *Mashetani* tu kwa hoja ya kwamba kijitanzu hiki hakijajitokeza katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Kwa mantiki hiyo basi kijitanzu hiki cha fasihi simulizi kinatofautisha uandishi wa tamthiliya ya *Mashetani* na tamthiliya za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Kijitanzu hiki cha wimbo katika tamthiliya ya *Mashetani* kinajitokeza pale mhusika Binadamu anapoimba kwa furaha hasa baada ya kufanikiwa kumuangamiza mhusika Shetani aliyekuwa akimkandamiza kwa muda mrefu. Kwa ufafanuzi zaidi tuangalie mfano ufuatao:

> Wako wapi walio wakijitapa?
> Sasa twawataka.
> Wako wapi walio wakijitapa?
> Sasa twawataka.
> Tumekwisha (anacheka) wakamata
> Wakamata.
> Tumekwisha wabwatabwata.
> Wako wapi waliokuwa juu jana?
> Sasa twawataka
> Wako wapi waliokuwa juu jana?
> Sasa twawataka
> Tumekwisha waangusha
> Waangusha.
> Tumekwisha wasagasaga
> Tumekwisha wakamata
> Wakamata.
> Tumekwisha wabwatabwata.
> Tumekwisha waangusha
> Waangusha.
> Tumekwisha wasagasaga (*Mashetani*, 1970:9-10)

Sehemu hii imejadili kwa kina tofauti ya vipengele vya fasihi simulizi kati ya tamthiliya ya *Mashetani, Ngao ya Jadi* na *Jogoo Kijijini.* Utafiti huu umebaini kuwa utofauti wa vipengele vya fasihi simulizi kati ya tamthiliya ya *Mashetani, Jogoo*

Kijijini na Ngao ya Jadi umejitokeza kupitia kipengele cha nyimbo na mianzo na miisho ya kifomula. Sehemu inayofuata tumejadili kwa kina namna vipengele vya fasihi simulizi vilivyotumiwa Hussein katika kuibua dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule.

4.3 Namna Vipengele vya Fasihi Simulizi Vilivyotumiwa Kuibua Dhamira Mbalimbali Katika Tamthiliya Teule

Utafiti huu ulilenga kubainisha dhamira zinazojitokeza kutokana na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi na Mashetani.* Utafiti huu umebaini kuwa, Hussein kwa kiasi kikubwa amefanikiwa kutumia vipengele vya fasihi simulizi kuibua dhamira mbalimbali katika tamthiliya hizi teule. Sehemu ifuatayo inabainisha dhamira zilizoibuliwa kutokana na matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini, Ngao ya Jadi na Mashetani*.

4.3.1 Dhamira zinazojitokeza katika tamthiliya ya Mashetani

Ebrahimu Hussein amaefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia vipengele vya fasihi simulizi katika kuibu na kuendelea dhamira katika tamthiliya hii. Sehemu ifuatayo inaonyesha dhamira zilizoibuliwa na vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya ya *Mashetani*.

4.3.1.1 Umuhimu wa Elimu

Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ameibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kupitia tashihisi. Hiki ni mojawapo ya kipengele cha kifasihi simulizi kilichotumiwa

na Hussein katika kuibua na kuendeleza dhamira ya umuhimu wa elimu dondoo lifuatalo linathibitisha hilo:

> **Juma:** Sasa unaniambia nini. Hujaniambaia kitu. Kweli inauma bwana. Kweli … acha yote hayo. Ukweli bwana, *degree inakupa tonge la wali na mchuzi, tena mchuzi wa kuku, badala ya tonge la ugali na maharagwe* (Mashetani, 1971:17).

Kauli hii ya juma imefumbata tashihisi ambapo kupitia tashihisi hii Hussein ameweza kuibua dhamira hii ya umuhimu wa elimu. Kupitia tashihisi hii tunapata kufahamu kuwa elimu humuwezesha mtu kuishi maisha mazuri ukilinganisha na mtu ambaye hana elimu. Hivyo basi Hussein anasisitiza kuwa ni muhimu kwa jamii kuwapatia vijana wao elimu tena elimu bora na siyo bora elimu kwani kwa kufanya hivyo taifa la kesho litaweza kupunguza kama si kuondoa kabisa makali ya maisha.

4.3.1.2 Ukoloni Mamboleo

Utafiti huu umebaini pia Hussein ametumia ishara zinazojitokeza katika ngano simulizi ya Chewa aliyoitamba bibi Juma kuibua dhamira ya ukoloni mamboleo. Ishara ni miongoni mwa vikale vinavyojitokeza sana katika fasihi simulizi za jamii mbalimbali duniani kote. Kwa kupitia kikale hiki Hussein ameweza kuijenga dhamira ya ukoloni mamboleo ambapo amemtumia mhusika Chewa kuashiria nchi za kimagharibi ambazo ziliwahi kulitawala bara hili la Afrika na kwa sasa linalitawala bara hili kwa aina mpya inayofahamika kama ukoloni mamboleo. Katika kuendeleza dhamira hii Huseein anatumia ishara Mkondo wa maji unaovuta mashua yoyote ile inayoitaka kuashiria namna nchi za kibepari zinavyoziendesha nchi za Kiafrika kupitia mfumo mpya wa kikoloni yaani ukoloni mamboleo. Japokuwa

wakoloni walifungasha vilago vyao mwishoni mwa miaka ya sitini lakini bado wanaendelea kuzitawala nchi za Kiafrika kupitia ukoloni mamboleo. Pia Hussein anatumia ishara ya mashua kuashiria nchi za dunia ya tatu ambazo zinaendeshawa na nchi za kibepari akadri zitakavyo. Kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> **Kitaru:** Hadithi ya Chewa. Mbali sana, ukivuka bahari saba, kuna chewa mkubwa. *Chewa* huyu akivuta *pumzi maji* yote yanakupwa, maji yote yanaingia kinywani mwake. Anaweza kutoka uko aliko, kuivuta na kuimeza *mashua* yoyote anayoitaka. *Mashua* inavutwa tu na *mkondo wa maji*, ikitaka isitake. (*Mashetani*, 1970:28).

4.3.1.3 Anguko la Ukoloni Mkongwe

Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumiwa wahusika wa kifasihi simulizi na ishara kuibua dhamira ya anguko la ukoloni mkongwe. Wahusika wa kifasihi simulizi waliotumiwa kuibua dhamira hii ni pamoja na mhusika binadamu na mhusika Shetani ambapo mhusika Shetani ametumiwa kuwakilisha mkoloni ambaye nanamkandamiza na kumuonea mhusika binadamu aliyetumiwa kuwakilisha Waafrika walikuwa chini ya utawala wa kidhalimu wa kikoloni. Kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> **Shetani:** Unajua mimi nani?
> Mimi shetani.
> Siyo jinni wala kuhani.
> Uwezo wangu hauifadhiki.
> Wema wangu hauhisabiki.
> Ubaya wangu hausemeki
> Ninajenga.
> Ninabomoa.
> Ninatukuza.
> Ninadhalilisha nitakavyo.
> Mimi ni nguvu na nguvu ni mimi.
> Mimi ni uwezo na uwezo ni mimi
> Unaniogopa
> **Binadamu:** Ndiyo
> **Shetani:** Unaninyenyekea?

> **Binadamu:** Ndiyo
> **Shetani:** (*kwa ukali*.) Njoo hapa! (*binadamu anakuja*) Sivyo, sivyo, sivyo! Sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio*.) Ah, sivyo hata kidogo. Jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa*.) Hebu jaribu tena. We, njoo hapa. (*Binadamu anakuja mbio. Akifika karibu, anakuja kwa kukwawa. Anasujudu*.) Ndiyo, sasa sawa. Hivi sawa sawa. (Mashetani, 1970:1-3)

Ingwa Mwafrika alikandamizwa na kunyanyaswa na mkoloni kwa miaka mingi lakini ilifikia pahala mkoloni alijikaanga na mafuta yake mwenyewe kwani kupitia elimu aliyoipata Mwafrika kutoka kwa mkoloni aliitumiwa kujikomboa toka katika makucha ya kikoloni. Katika tamthiliya hii Hussein ametumia kisu kuwakilisha elimu ya kikoloni ambapo mhusika binadmu alikitumia kisu kumuulia shetani au kwa maneno mengine binadamu alitumia elimu aliyoipata kutoka kwa mkoloni kujikomboa. Hivyo basi kifo cha Shetani kikawa ndiyo angko la mkoloni katika nchi za Kiafrika kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> Shetani na binadamu wanatazamana. Wote wanatabasamu. Shetani anampa Binadamu kisu. Wanashikana kama ndugu wawili wapenzi. Shetani anamwekea Binadamu ubavu sawa. Binadamu anatumbukiza kisu katika mbavu. … Shetani anaanguka. Binadamu anapumua anautazama mzoga
> **Binadamu:** Amekufa! Nimemuua! Nimemuua! (*Mashetani*, 1971:8)

4.3.1.4 Malezi Mabaya

Hussein ametumia wahusika wa fasihi simulizi katika kuibua dhamira hii. Mhusika aliyetumiwa na mhusika bibi na mhusika mama, hawa ni wahusika wanaojitokeza sana katika katika ngano simulizi za jamii mbalimbali duniani kote kwa mantiki hiyo basi mhuiska bibi ni mhusika kikale. Mhusika bibi amechorwa kama mhusika

anayemdekeza mjukuu wake kupita kiasi na kuimdekeza huko ndiko kunakopelekea kuharibika kitabia kwa mhusika Juma kwani kila Mama Juma anapojaribu kumkanya kijana wake kwa kumpa muongozo mwema kimaisha mhusika bibi anakuwa mkali kwa ithibati zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> **Mama:** Juma; ebu nitazamie hapo kama chungu change kinachenmka.
> **Juma:** Haya.
> **Mama:** Ebu nitazamie basi.
> **Juma:** Ndiyo.
> **Mama:** (baada yua muda) Sasa wewe Juma, husikii siyo? Umejipachika hapo viguu juu kama ndege; ukisemeshwa hujibu. Hata huyo korongo anatua chini kudondoa samaki.
> **Bibi:** Hm. Mwache ajisomee saa. Kikichemka mimi nitakwambia. Mimi nakiona kwa hapa.
> **Mama:** Acha tumseme. Ukimfanyia hivyo ndivyo anazidi kichwa. Anajidekeza kama nini kwako huyo. Kaharibika siku hizi kama nini. Siku ile hapa nili…
> **Bibi:** Chungu chako kinachemka. Mwanamke huachi mdomo. Ke, ke, ke, kama cherehani. Namna gani? Tabia mbaya (mama anachukua nazi yake aliyokuna, mbio anakwenda jikoni. Akipita karibu ya Juma anajigonga)
> **Mama:** Mamaaa! Ayi! Ayi! Ayii! Mungu wangu. Na hivi viti mnaweka mlangoni, hamuweki mahali pengine.
> **Juma:** Sasa mimi niweke wapi? Nafasi yenyewe iko wapi?
> **Bibi:** (kwa sauti ya kusengenya) Nyamaza. Jisomee hapo. Unamsikiliza mwendawazimu huyu? We nyamaza tu. (Baada ya muda)
> **Mama:** (anatoka jikoni) Nimesikia, nimesikia yote mliyoyasema. Lakini mimi kweli nitasema. Juma siku hizi umekuwa na roho mbaya. Siku ile mama yake Kitaru alikuja hapa, akasema, 'Kitaru mgonjwa. Anaumwa.' Mimi nikauliza, 'anaumwa?' 'Ndiyo anaumwa' Nikasema, 'Akija Juma nitamwambia'. Haya. Akaja Juma hapa. Mimi nikamwambia, 'Juma rafiki yako anaumwa.' Huyo mwenyewe, muulizeni kama ninamsingizia. Akajibu, 'Nimesikia.' Basi, nimesikiiiaaa. Haramu kama mtoto alinyanyua unyayo … unyayo bibi. Kaganda hapo hapo juu ya kiti kama mfalme. Sema! Uwongo? Aah nisute.
> **Bibi:** Sasa hakwenda, si basi. Wewe kinakuhusu nini? Labda mwenyewe ana sababu zake. Utajuaje? Kwani huyo kitaru rafiki yako wewe au rafiki yake yeye? Au wewe ulijuaje kama hakwenda?

> **Mama:** Rafiki yake yeye. Lakini tunamwambia tu, mwendo anaokwenda siyo. Siyo mwendo mzuri. Siyo mwendo wa kiwatu. Watu hawafanyi hivyo.
> **Bibi:** Hayo usiyaseme. Mambo ya kiwatu sijui. Mambo ya nini sijui. Hayo usiyaseme. Huyo kitaru, aliyekuwa mtu, mbona mimi hapa sijamuona…? Mbona mimi sijamuona? Leo wiki ya ngapi hii?...Kaa baba… (Baada ya muda Juma anakurupuka anatoka nje.)
> **Mama:** Haya tazama kiburi hicho. Tumemsema kidogo, huyoo kachomoka. Maana yake sisi wapuuzi.
> **Bibi:** Afadhali aondoke. Ikisha hwishi kumsumbua aah. Afadhali aondoke. Mtoto asirudi nyumbani. Akirudi tu kwe, kwe. kwe, kwe, kwe, kwe, kwe, kwe, Hm. Pole basi tena.
> **Mama:** Kumsema tutamsema … mtoto kiburi kimempita kimo.
> **Bibi:** Uss! Funga mdomo. Alaa! Na mimi utanipa hishima yangu. Nikusikie tena tu kumzulia Juma uwongo… basi haram utaona. Alaa! Mtoto hana raha… (*Mashetani*, 1971:36-39).

Anachokifanya Bibi Juma katika hakika si mapenzi bali ni uharibifu kwani kimsingi motto anapokosea mzazi anapaswa kumkosoa na kumuonysha njia impasayo kuifuata lakini Bibi Juma hayuko tayari kuona Mama Juma akimkanya kijana wake yeye anaona kuwa mama hatendi haki bali anamuonea mjukuu wake. Ingawa Juma anaonekana kuwa sambamba na anachokisema Bibi yake lakini baadaye anakaa chini na kutafakari na kung'amua kuwa anachokifanya bibi yake si mapenzi bali ni uharibifu kama mwenyewe anavyosema:

> Bibi anapuliza sumu.
> Sumu au mapenzi?
> Jaribu kupambanua:
> Mapenzi hugeuka sumu.
> Naam, mara nyingi
> Mapenzi hugeuka sumu (*Mashetani*, 1970: 42).

4.3.1.5 Imani za Kijadi

Hussein ametumia mbuyu kuibua dhamira ya imani za kijadi. Mbuyu ni kikale ambacho hutumiwa na watambaji wa ngano simulizi kurejelea pahala patakatifu

panapoishi wahenga na wakati mwingine mbuyu hutumiwa kurejelea pahala panapoishi mashetani au majini ambayo hudhuru watu. Katika tamthiliya hii mbuyu umetumiwa kuashiria pahali panapoishi mashetani yanayodhuru binadamu. Mama Kitaru alilifahamu hili na ndiyo maana aliamini kuwa kijana wake amekumbwa na shetani na hii inatokana na ukweli kwamba Kitaru alikuwa akicheza na Juma Mbuyuni ambapo kwa imani ya mama Kitaru ni pahala hatari kama mwenyewe anavyosema:

> Namuogopea Kitaru. Mimi nafikiri kakumbwa na shetani maana hawa wanakwenda kucheza mbuyuni, ule mbuyu mkubwa. Na mimi ninajua ule mbuyu mbaya. Una hatari kweli kweli. (Mashetani, 1971:27)

4.3.2 Jogoo Kijijini

Utafiti huu umebaini kuwa katika tamthiliya ya *Jogoo Kijijini* Hussein ametumia ushairi, tashihisi, ishara kuibua dhamira ya ukandamizaji, anguko la matabaka na kujitoa mhanga. Sehemu inayofuata inajadili kwa kina dhamira tajwa hapo juu.

4.3.2.1 Ukandamizaji

Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumia ishara katika kuibua dhamira hii ya ukandamizaji ambapo anatumia neno *nyayo* kuashiria nchi za Kiafrika zilizokuwa zikikandamizwa kwa kunyiwa uhuru wao wa kujiamulia mambo yao na kuishi watakavyo. Na neno *Kiatu* limetumiwa na Hussein kuashiria mfumo wa kiutawala wa kikoloni uliokuwa ukiwakandamiza Waaafrika wakati wa utawala wa kikoloni. Katika kuendeleza dhamira hii Hussein ametumiwa neno *sikio* kuashiria mkoloni aliyekuwa akijifanya kiziwi kwa kutokusikiliza malalamiko ya *unyayo* (Waafrika) ambao walikuwa wamechoshwa na utawala wa kidhalimu wa kikoloni kwani

walikuwa wametawaliwa kwa miaka nenda miaka rudi. Ingawa *sikio* linajifanya halisikii lakini kiuhalisia linasikia kwa maana lingekuwa halisikii lisingesikia *upepo upitao njia* yaani vugu vugu la mabadiliko. Baada ya vita ya pili ya dunia nchi nyingi nzilizokuwa chini ya utawala wa kidhalimu wa kikoloni zilisimama kidete kudai uhuru wao japokuwa wakoloni hawakuwa tayari kuzipa nchi hizo uhuru wake lakini walifahamu fika kuwa dunia imekumbwa na mabadiliko wa watawaliwa waliyaona hayo mabadiliko na ndiyo maana wakadai uhuru wao kwani walikuwa wamekwisha choshwa kutawaliwa kwa ufafanuzi zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

Mtu
‘*Nyayo* kisogoni
Jicho ardhini
Ulimi kinywani
Ukihisabu hatua za hatima
Baina ya unyayo
Karibu na sikio
Auishi ya malalamiko
‘Nyayo litamka
‘Ewe sikio sikia;
Mimi mahabusu wa myaka
Wa *k’yatu* ulichonivika
Gizani ninadhohofika
Nataka ona *juwa* la siku njema
Nimechoka thama ‘mechoka
Najua *jogoo awika*
Lakini mi *nakwaruzika*
Katika *giza* lisilo ‘nufaiya
Humu k’bandani *kiyatuni*
Naishi *gizani* tabuni
Nachunika mikwaruzoni
Ninapopambana na hii dunia
Lakini sikio,
Lilikuwa sikio la kufa
Hasha
Aslani halikufa
Ingekuwa sikio limekufa
Singelewa upepo pitao njia (*Jogoo Kijijini*, 1976:15-16).

4.3.2.2 Anguko la Matabaka

Matabaka ni mojawapo ya tatizo kubwa linalozikabili nchi nyingi za Kiafrika kwani jamii zimekuwa zikijinasibisha na tabaka zao na kusahau utaifa wao na hii ilitokana na ukoloni ambao ulijali sana nasaba kuliko utaifa na kuwagawa watu kulingana na nasaba zao. Lakini mwanzaoni mwa mika ya sitini na mwishoni mwa miaka ya sabini nchi nyingi za Kiafrika zilipata uhuru wao kutoka katika makucha ya kikoloni na viongozi wa nchi zilizojipatia uhuru wao wakaanza kufutilia mbali matabaka. Katika kulionyesha hili Hussein anatumia ushairi uliofumbata ishara kuibua dhamira hii ambapo ametumia neno mlango kuashiria matabaka yaliyoasisiwa na kuendelezwa na utawala wa kidhalimu wa kikoloni na uchwa *shababi* kuashiria viongozi wazalendo wenye uchungu na nchui zao waliofanya jitahada kubwa ya kuahakikisha kuwa ubwana na utwana unakomeshwa katika mataifa yao machanga. Kwa ithibati zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

> Lakini
> Mlangoni
> Mbuubuu ukatambaa
> kwa
> hiyo
> Uchwa shababi
> Mlango waliushambulia
> Na mbele ya uchwa janabi
> Nasaba ikang'wenyeka
> Ubwana 'kapukusika
> Utwana 'kap'perushika
> Halafu ndiyo utu
> Katika rutuba ukajiotea (Jogoo Kijijini, 1976:21)

4.3.2.3 Kujitoa Muhanga

Mbadiliko yoyote yale katika jamii hayawezi kupatikana kama watu hawatakuwa tayari kubeba makosa yaliyofanywa na waliowatangulia ili kuleta mabadiliko

yatakayoinufaisha jamii. Suala hili linahitaji mtu aliyetayari kujitoa mhanga kwa manufaa ya vizazi vijavyo. Hussein amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia utanzu wa ushairi kuibua dhamira ya kujitoa muhanga ambapo amemtumia muhusika Kijana ambaye baada ya kuambiwa na ajuza kuwa matatizo yote wanayoyapata yametokana na makosa waliyoyafanya wao kawani walipota madaraka waliwasahau waliowafikisha hapo walipo na kuwadharau na kujenga ukuta baina yao na wazawa. Baada ya kijana kuufahamu ukweli huo anakubali kubeba madhambi yote yaliyotendwa na kizazi kilichomtangulia kama anavyosema mtambaji:

> Kijana kuusikia ukweli
> Hata hakuhuzunika asili
> Mabega yake wasaa mawili
> Yalibeba madhambi ya ile njia
> Ikaonekana
> Ikaonekana kwamba
> Kwamba ililazimika fidia *(Jogoo Kijijini, 1976:28-30)*

4.3.3 Ngao ya Jadi

Utafiti huu pia umebaini kuwa Hussein ametumia wahusika wa kifasihi simulizi, ushairi, tashihisi na mtambaji kuibua dhamira ya anguko la ukoloni mkongwe, Unyonyaji na ukandamizaji. Hivyo basi sehemu hii imewasilisha kwa kina ufafanuzi wa dhamira hizi.

4.3.3.1 Unyonyaji na Ukandamizaji

Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumia kikale cha ushairi na ishara kuibua dhamira ya unyonyaji na ukandamizaji. Katika kuendeleza dhamira hii Hussein ametumia mhusika kikale Joka Sesota kuashiria ukoloni mkongwe uliokuwa

ukizikandamiza nchi za kiafrika kwa kuzinyonya kwa ithibati zaidi tuangalie dondoo lifuatalo:

Kwani
‘Likuwa tabia makini
Killa mwaka ukibaini
Joka hushuka kijijini
Kuchukua mali na binti Mwema mmoya
Tena lilikuwa fisadi
Mali ya watu tangu jadi
Nao watoto wa Wadudi
Na mshenzi maluuni kuchukuliwa! *(Ngao ya Jadi, 1976:35-36)*

4.3.3.2 Anguko la Ukoloni Mkongwe

Utafiti huu umebaini kuwa Hussein ametumia kikale cha ushairi kuibua dhamira ya anguko la ukoloni mkongwe ambapo anguko la ukoloni mkongwe lilitokana na Waafrika kuchoshwa na unyonywaji uliokuwa ukifanywa na utawala wa kikoloni na hivyo kuamua kumteua mtemi ambaye alijitoa mhanga kupambana na Joka Sesota na kufanikiwa kulisambaratisha. Kuondolewa kwa mkoloni kuliwafanya Waafrika kushangilia kwa shangwe kubwa kama asemavyo mtambaji:

Basi hapo
Mtemi akaja karibu
Akasogea
Kwa uchungu na ghadhabu
Na kwa ushujaa wa ajabu
Lile jiti panda mbali kaling’olea
Karusha ngao angani
Jiti, kabana kwapani
Ile ngao
Ikampaisha angani
Yeye na lile jiti panda pamoya
Na angani
Shuwarini
Lile Joka kalibaini
Shingoye kwa utuvu akaipimiya
Lile jiti akaligeuza
Pandake chini ikachomoza
Kimbelembele ikaongoza

Shingo la Joka chini kaipigilia
Hapo katoka yowe
Na vingi vigelegele
Nd'o kina dada wale
'Lipiga wapigavyo
Azaliwapo mtoto dume mmoya
Sesota
Likapiga mikambi yake
Likatoa kelele zake
Miti yote karibu yake
'Kivuruga kasha likatokomeya
Kaingia kitongojini
Shuwari na nyingi amani
Watu wakawa furahani
Watu wote kitongojini killa mmoya
Nyunyusa
Ngomaze 'kazikaanga
Kina dada
Vibwebwe 'kavifunga
Nyunyusa
Ngomaze kazigonga
Vyuma, viuno vinonono 'kajikatia
Shaaba Roberti
Uwanjani 'kajikita
Mathias Mnyapala
Swahibuye 'kamwita
Kezilahabi, Muyaka
Wote wakaitika
Watu nd'o kwa ngonjera wakajileweya
Pia Penina Muhando
Hasa Ngungi wa Thiong'o
Abdilatif si 'wongo
Kwa hii michezo wakatutumbuizia
Na akina hohehahe hawa
Kabwela kina Hussein hawa
Na'o mashetani wakajawa
Wakapungwa na madadi wakaingiwa (*Ngao ya Jadi*, 1976:44-45)

4.4 Hitimisho

Sura hii imewasilisha data kwa mujibu wa malengo mahususi ambayo yalikuwa matatu. Tumefanikiwa kubainisha namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyozitofautisha na kuzifananisha tamthliya teule Pia, tumebainisha dhamira

zilizoibuliwa na vipengele mbalimbli vya fasihi simulizi tulivyovibainisha katika tamthiliya teule.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ndiyo sura ya mwisho katika utafiti huu ambayo imefanya kazi ya kuhitimisha utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ya sura hii inahusu muhtasari wa utafiti huu, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu ambayo inajumuisha malengo mahsusi matatu yaliyouongoza utafiti huu. Malengo hayo yamefafanuliwa kimuhtasari kuonyesha namna yalivyoshughulikiwa na kuweza kufikiwa na kukamilishwa kikamilifu. Kwa mantiki hiyo basi, malengo hayo yameweza kutimiza adhma ya kutekelezwa utafiti huu. Na sehemu ya tatu inatoa mapendekezo kwa tafiti zijazo kuhusiana na maeneo yaliyogusiwa na utafiti huu kwa ujumla.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu una jumla ya sura tano. Sura ya kwanza imefafanua kwa kina vipengele vinavyounda utangulizi wa utafiti huu. Vipengele hivyo ni muhtasari wa tamthiliya teule, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambayo yamejumuisha lengo kuu na malengo mahsusi. Vipengele vingine ni maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake pamoja na mipaka ya utafiti na mwisho ni hitimisho.

Sura ya pili imefafanua kwa kina maandiko mbalimbali ya kazi tangulizi kuhusu ufasihi simulizi unaojitokeza katika matini mbalimbali za fasihi kwa ujumla na

kubaini yale yaliyokwisha kutafitiwa katika mada hii. Pia katika sehemu hii tumedhihirisha pengo la utafiti ambalo ndilo lililoshughulikiwa katika utafiti huu.

Sehemu hii pia imejadili kwa kina nadhariya zilizotumika katika uchambuzi wa data ambazo ni nadhariya ya vikale na nadhariya ya Fasihi Linganishi. Vilevile tumebainisha namna nadhariya hizi zilivyotumika katika uchambuzi wa data. Nadhariya ya Fasihi Linganishi imetumika katika kufanikisha zoezi zima la kulinganisha na kulinganua ufasihi simulizi uliotumiwa na Hussein katika ujenzi wa tamthiliya teule. Na kwa upande wa nadhariya ya Vikale, nadhariya hii imetumika kuchunguza dhamira zilizojitokeza katika tamthiliya teule.

Katika sura ya tatu, tumeeleza kwa kina njia na mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa. Vipengele vinavyounda sura hii ni pamoja na usanifu wa pendekezo la utafiti, eneo la utafiti, populesheni, usampulishaji na sampuli ya utafiti, vyanzo vya data vinavyojumuisha data ya msingi na data ya upili, mbinu za ukusanyaji data, mbinu ya uchambuzi wa data, kuaminika kwa matokeo ya utafiti, usahihi wa data, maadili ya utafiti na kipengele cha mwisho ni hitimisho.

Sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data pamoja na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo zinaakisi maswali ya utafiti ambayo ndiyo yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza imejadili juu ya vipengele vya Fasihi Simulizi katika tamthiliya teule. Sehemu ya pili imejadili imejadili kwa kina namna vipengele vya fasihi

simulizi vinavyoibua na kuendeleza dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule na mwisho kuna hitimisho.

Sura ya tano imewasilisha muhtasari wa utafiti, hitimisho na kisha kutoa mapendekezo kwa watafiti watakaopenda kufanya utafiti katika maeneo yanayohusiana na ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili.

5.3 Hitimisho

Kwa ujumla, utafiti huu umefanikiwa kukamilisha malengo yake mahsusi ambayo yalikuwa matatu. Lengo mahsusi la kwanza lililenga Kulinganisha vipengele vya Fasihi Simulizi katika tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Na lengo mahsusi la pili lilikusudia kutofautisha vipengele vya fasihi simuliz katika tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*. Na kwa upande wa lengo la tatu lilijikita katika kubainisha namna vipengele vya fasihi simulizi vinavyoibua na kuendeleza dhamira mbalimbali katika tamthiliya teule.

5.3.1 Vipengele vya Fasihi Simulizi katika Tamthiliya Teule

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kwamba kuna ufanano mkubwa wa matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya za *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Ufanano huo umejidhihirisha kupitia vipengele vya fasili simulizi vya matumizi ya ngano, mtindo wa ishara, matumizi ya wahusika wa fasihi simulizi, matumizi ya mtambaji na kuchanganya tanzu. Kwa upande wa kuchanganya tanzu Hussein ametumia ushairi, majigambo na tashihisi katika tamthiliya zote tatu.

5.3.2 Kutofautiana kwa Vipengele vya Fasihi Simuliz katika Tamthiliya Teule

Utafiti huu umebaini kuwa ingawa kuna mfanano mkubwa wa vipengele vya fasihi simulizi kati ya tamthiliya ya *Mashetani, Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* lakini kufanana huku kwa vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya hizi teule hakumaanishi kuwa hakuna tofauti ya vipengele vya fasihi simulizi katika tamthiliya hizi teule. Utofauti huo wa vipengele vya fasihi simulizi umejitokeza kupitia kipengele cha nyimbo na mianzo na miisho ya kifomula.

5.3.3 Dhamira Zinazojitokeza katika Tamthiliya Teule

Utafiti huu umebaini kuwa, Hussein kwa kiasi kikubwa amefanikiwa kutumia vipengele vya fasihi simulizi kuibua dhamira mbalimbali katika tamthiliya hizi teule. Hussein ametumia nyimbo, ushairi, mianzo na miisho ya kifomula, ngano, mtindo wa kuchanganya tanzu, majigambo, ishara, wahusika wa fasihi simulizi, tashihisi na mtambaji kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu, ukoloni mamboleo, anguko la ukoloni mkongwe, malezi mabaya, imani za kijadi, kujitoa mhanga, anguko la matabaka, unyonyaji na ukandamizaji.

5.4 Mapendekezo

Kwa watafiti watakao penda kufanya utafiti juu ya ufasihi simulizi katika tamthiliya ya Kiswahili tunapendekeza kuwa, tafiti zao zijikite zaidi katika kutafiti ulinganisho wa ufasihi simulizi kati ya tamthiliya za Ebrahimu Hussein na waandishi wa baadaye mathalan, Emmanuel Mbogo na wengineo.

MAREJELEO

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*. (2nd Edition). London: Oxford Univerity Press.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research: Statistics and Measurement*, Department of Distance Education Institute of Adult and Continuing Education Makerere University, Kampala.

Good, G. V. (1966). *Essentials of Educational Research*. New York: Maridth Publication Co.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Hussein, E. (1970). *Wakati Ukuta*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Hussein, E. (1970). *Alikiona*. Dar es Salaam: East African Publishing House.

Hussein, E. (1973). *Mashetani.* Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E, (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Nairobi: Oxford University Press.

John, L. (2007). "Critical Reading: A Guide." In http://www.brocku.ca/English/jlge/criticalreading.html. Accessed on 30th Nov. 2007.

King'ei, G. K. (1987). "Usanifu wa Lugha katika Uandishi wa Ebrahim Hussein," *Mulika*, Na. 19, TUKI, Kur.19-35.

Kombo, D.K & Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing*: *Introduction,* Nairobi: Pauline Publication Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Koithari, C.R (2014). *Research Methodology Methods and Techniques* (3rd Revised Edition). New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kuria, H. (1957). *Nakupenda Lakini*…Nairobi: East African Literature Beaure.

Maina, K. P. J. (2013). “Athari za Fasihi Simulizi katika Riwaya ya Utubora Mkulima,” Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mbatia, M. (1990). “Mbinu za Uandishi katika Riwaya za Mwanzo za Shaaban Robert,” Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Cha Nairobi, Nairobi, Kenya.

Mbogo, E. (2008). *Sundiata*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mbogo, E. (2015). *Sadaka ya John Okello*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Mbogo, E. (2015). *Nyerere na Safari ya Kanani*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Mbogo, S. & Wenzake. (2012). Research Methodology, Open University of Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

Mohamed, S. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1992). *Msingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publisher.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mhando, P, (1973). *Tambueni Haki Zetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Limited.

Mhando, P. (1975). *Pambo*. Dar es Salaam: Foundation Books.

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mhando, P. (1984). *Lina Ubani*. Press, Dar es Salaam: Dar es Salaam University.

Mkwera, F. R. F (1977). "Ebrahim Hssein Mwandishi wa Tamthiliya." katika *Mulika* Na. 11, TUKI, Kur. 38-45, Dar es Salaam.

Newman, W. L. (2006). *Social Research*. (6th Edition). Boston: Pearson.

Ngugi, G, (1961). *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* Nairobi: East African Literature Beaure.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K & Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nicholaus, A. (2011). "Falsafa ya Ubuntu ilivyosawiriwa katika Tamthiliya teule za Penina Muhando," Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ponera, A. S. (2014). ''Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi'' Tasnifu ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Robson, C. (2007). *How to do a Research Project: A guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Salim, M. (2015). "Kuchunguza Ufasihi Simulizi unaojitokeza ndani ya Hadithi ndefu za Kusadikika na Adili na Nduguze," Tasinifu ya M.A, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Samwel, M. (2013). *Tamthiliya ya Kiswahili: Kutoka Miviga ya Kidini hadi Filamu*, MEVELI PUBLISHERS (MVP), Dar es Slaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam : KAUTTU Limited.

Simiyu, W. F. (2011). *Kitovu Cha Fasihi Simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*, Mwanza: Serengeti Bookshop.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Focus Publications Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi Vide: Muwa Publishers Limited.